SportPesa
TZS. 878,152,880
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Wawili mbaroni tuhuma za mauaji ya mwanamke**

UKURASA 3




UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Januari 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580837

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Wamachinga Dar sasa kujengewa masoko ya kisasa

• **Samia** awaruhusu kurejea Karume, vitambulisho vyao kuboreshwa...

*Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wafanyabiashara wadogo maarufu machinga katika soko la Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam, wakianza ujenzi wa mabanda yao jana, baada ya kuruhusiwa kujenga ili waendelee na biashara kutokana na soko hilo kuungua moto hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MITAALA MIPYA YA ELIMU RASMI 2025**

SERIKALI imesema mitaala mipya ya elimu kuanzia elimu ya awali, msingi...

UKURASA WA 4

**KESI YA KUJIUZULU NDUGAI KUANZA LEO**

JOPO la majaji watatu leo linatarajia kuanza kusikiliza kesi ya kikatiba...

UKURASA WA 8

**DEWJI AZIDI KUNG'ARA ORODHA YA MABILIONEA**

LICHA ya mlipuko wa virusi vya corona, mabilionea wa Afrika wameongeza...

## Japan yaisaidia TRA vifaa kuzuia upotevu wa mapato

UKURASA 4



## Madaktari bingwa 11 wa China watua nchini

UKURASA 3

**MICHEZO** MOALLIN KOCHA MKUU KAMILI AZAM UK.20

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Machinga kujengewa masoko ya kisasa Dar

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali inatarajia kujenga masoko ya kisasa yenye miundombinu yote ambayo wafanyabiashara wadogo (machinga) watafanya biashara zao kwa saa 24.

Alitoa kauli hiyo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na viongozi wa machinga mkoani humo, likiwa ni agizo lake kwa mkoa kukutana nao.

Rais Samia alisema: "Nimeambiwa mna kanzi data nzuri, tutaweka mifumo ya mitandao katika masoko, tunajitahidi kutafuta maeneo mengine ya wazi yakiwamo mliopendekeza ili tuweke masoko pembezoni mwa jiji, tunahangaika kutafuta fedha za ndani na nje, hata kama tutakopa, tutarejesha."

Rais Samia alisema lengo la ujenzi wa masoko hayo ni kuwawezesha machinga kufanya shughuli zao kwenye maeneo yenye miundombinu iliyoboreshwa, ambayo itawawezesha kuwa wafanyabiashara wakubwa na kuchangia pato la taifa katika ulipaji wa kodi.

"Mwenyekiti wenu amesema hapa: 'Ndiyo tumehama na tumepangana, lakini kuna wenzetu wamekosa maeneo' hili tunalitambua kwa maana hiyo juzi nilikutana na Mkuu wa Mkoa (Amos Makalla), nikamwambia nendeni kawekeni mipango mizuri Karume (soko lililoteketea kwa moto) lakini acha machinga warudi haraka Karume.

"Niliamua hivyo nikijua kwamba kukaa kwenu nje kuna matatizo mengi, biashara haifanyiki familia zinasubiri, nikasema pamoja tuna lengo la kujenga masoko mazuri lakini siyo sasa kwa Karume, waachiwe warudi, kawaombe wajijengee vibanda baadaye tutakuja kushughulikia."

Rais Samia alifafanua kuwa ametoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Kariakoo ambalo litajengwa kwa miezi 18, kwamba likikamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua wafanyabiashara zaidi ya 4,000.

"Hatua ya pili, nimemwambia Mkuu wa Mkoa twende tukajenge eneo la Jangwani na fedha za kuanzia zipo, nimemwambia aingie kwenye hatua ya manunuzi, atafute mkandarasi atakayetujengea Jangwani kwa ramani ambayo (machinga) mtashirikiana na kukubaliana," alieleza.

Rais Samia alisema baada ya Soko la Jangwani kukamilika, wataelekea Soko la Karume kwa sababu ni lazima katikati ya Jiji la Dar es Salaam kuwe na masoko yenye miundombinu na huduma zote na yatafanya kazi usiku na mchana.

**AIPA TAFU SACCOS**

Aidha, Rais Samia aliwaahidi machinga kuwa atakutana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuangalia namna watakavyozigawa Sh. bilioni tano za UVIKO-19 ili nao wapate sehemu ya fedha hizo zitakazoingizwa kwenye Saccos yao waliyoianzisha. Kuhusu ombi la kuanzishwa kwa madawati maeneo mbalimbali, Rais Samia alisema amelipokea na kuahidi kuzungumza na mamlaka husika, ikiwezekana kundi hilo liingie katika Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu ambako sera za machinga inaweza kutungwa.

**AWAAGIZA WAKURUGENZI**

Kadhalika, Rais Samia aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kuweka mipango maalum ya namna asilimia 10 ya fedha zilizotengwa maeneo yao zitakavyolinufaisha kundi hilo.

"Ninataka wakurugenzi katika bajeti zenu mtenge fungu maalum litakalosaidiana na fedha zinazotafutwa na serikali katika kuboresha maeneo ya machinga, hiki kitakuwa kigezo kimoja wapo katika kazi zenu," aliwaeleza.

Katika hatua nyingine, Rais Samia ameahidi kuliangalia pendekezo la machinga kwa Shirika la Nyumba (NHC) walilotaka lijikite katika kutengeneza maeneo ya biashara ambayo watawapangisha.

Pia aliiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kulishughulikia kwa haraka tatizo la njia kwenye maeneo ambayo machinga wamehamishiwa ili daladala ziweze kufika.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, Ikulu jijini Dodoma juzi.
**PICHA: IKULU**

# ...Rais Samia kuboresha vitambulisho vyao

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameahidi kuviboresha vitambulisho vya machinga kwa kuvitengeneza vipya ambavyo vikiingizwa kwenye mashine vitatoa taarifa zao na kuwawezesha kupata huduma sehemu yoyote.

Alitoa ahadi hiyo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na viongozi wa wafanyabiashara wadogo (machinga).

Rais Samia alisema vitambulisho hivyo vitawawezesha kwenda sehemu yoyote, vitawafaa kufanya navyo kazi au kupata huduma.

"Kitambulisho ambacho kitakuonyesha wewe ni nani, sasa hili tunasubiri tumalize sensa ya watu na makazi na mbali ya sensa tunasubiri maeneo ambayo tumeamua kuyajenga kwa sasa, kama Kariakoo, Jangwani na Karume, tutakapotoa kitambulisho tunamjua Lusinde kituo chake cha kazi ni Jangwani, ana miaka hii, biashara yake ni hii, ana watoto hawa," alisema Samia.

Alisema hawataharakisha kuvitengeneza kwa sababu vitakuwa vya gharama, hivyo amewataka wamachinga kuwa na subira ili vikitengenezwa viwe vyao daima.

Pia aliwaomba baada ya maboresho hayo kundi hilo lilipe kodi kwa kadri ya biashara zao ili serikali iendelee kuboresha miundombinu yao na kutoa huduma.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa machinga kulitazama suala la wenye maduka kuwapa machinga bidhaa zao ili kuwauzia kwa sababu mwenye kodi akipita dukani, mashine za EFD's hazionyeshi mauzo kwao.

Akizungumzia mchakato wa kuwapanga kwa kuwaondoa maeneo yasiyo rasmi, Rais Samia alisema kuna watu walisubiri vurugu zitokee, nchi iharibike lakini machinga wa Dar es Salaam walikuwa waungwana na wazalendo.

Pia alitoa pole kwa machinga baada ya kutokea kwa tukio la moto katika masoko ya Kariakoo na Karume.

Alisema Soko la Kariakoo lilipoungua sababu ilitajwa ni umeme na Karume taarifa za awali ni mshumaa.

"Lakini, moto unapoendelea hata magari ya kuzima moto yanapofika yanakosa sehemu ya kupita, mtakaporudi Karume mjipange ili itakapotokea hitilafu magari yaweze kupita na kuuzima," alisema Samia.

Rais Samia alisema serikali inawatambua machinga katika mipango yote inayopanga ukiwamo mpango wa miaka mitano uliomalizika, wa pili na wa tatu ambao chini ya Hayati Rais John Magufuli aliwatambua kwa kutengeneza vitambulisho.

Aidha, Rais Samia aliwataka wakurugenzi, wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia maslahi ya machinga na kuendelea na mchakato na kuyafanyia kazi matatizo yao.

## Mitaala mipya elimu rasmi 2025

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imesema mitaala mipya ya elimu kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu inatarajiwa kuanza kutumika Januari mwaka 2025.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Aneth Komba, aliyesema hayo jana jijini hapa alipokuwa akiwasilisha mada ya mitaala na kupokea maoni ya wadau ya kuboresha mtaala huo.

Alisema kwa sasa kazi ya kukusanya maoni ya wadau kwa ajili ya kufanya mapitio ya sita ya mitaala yanaendelea.

Hata hivyo, alisema mitaala inayotumika kwa sasa bado inafaa licha ya baadhi ya mambo yanaangaliwa kwenye mapitio ili yaongeze na yaendane na karne ya 21.

Kadhalika, Dk. Komba alisema ni vyema wasimamizi wa elimu kuhakikisha wanauelewa mtaala wa sasa kwa kuwa bado utaendelea kutumika hata baada ya kuanza kutumika mtaala mpya.

Wakitoa maoni yao kwenye mkutano huo, wadau hao walishauri masuala mbalimbali ikiwamo wahitimu wa darasa la saba waruhusiwe kuchagua kujiunga na elimu ya ufundi na siyo sekondari pekee.

Mratibu wa Elimu Dayosisi ya Arusha, Lushuru Sambwet, alishauri serikali kuangalia namna wanafunzi wanaohitimu darasa la saba kuwa na uchaguzi wa kujiunga na elimu ya ufundi na wengine kuendelea na sekondari.

Mkuu wa Shule Faraja maalum kwa watoto wenye ulemavu wa viungo, William Kivinyo, alishauri somo la lugha ya Kiingereza kuanza kufundishwa kuanzia elimu ya awali badala ya utaratibu wa sasa wa somo hilo kuanza kufundishwa kwa wanafunzi wa darasa la tatu.

Mwalimu wa Shule ya Lake Victoria, Juma Jackson, alishauri somo la stadi za kazi ambalo linafundishwa katika shule za msingi pekee lifundishwe pia kwa wanafunzi wa sekondari kuanzia kidato cha kwanza na cha nne.

# Madaktari bingwa 11 Wachina watua nchini

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imepokea timu ya madaktari bingwa 11, kutoka Serikali ya China waliobobea katika magonjwa ya ubongo, mishipa ya fahamu, mifupa, dawa za usingizi, ganzi na moyo.

Madaktari hao watafanya kazi nchini kwa miaka miwili, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya(MZRH).

Ujio wa madaktari hao nchini ni kupitia mkataba ulioingia Wizara ya Afya na Serikali ya China Septemba, mwaka jana wa ushirikiano wa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na kuleta madaktari bingwa kutoka nchini humo kutoa huduma katika hospitali za kibingwa nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, wakati wa kuwapokea madaktari hao, Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Dk. Vumilia Liggyle, alisema ushirikiano baina ya serikali hizo mbili ni wa kihistoria kwa sababu una zaidi ya miaka 50.

Alisema ushirikiano huo umekuwa ukiwanufaisha wataalamu kwenda nchini China kupata mafunzo na madaktari bingwa kutoka nchini humo kuja Tanzania kutoa huduma.

"Tumepokea jumla ya madaktari bingwa 11 kutoka China, watatoa huduma za kibingwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa miaka miwili katika hospitali zetu nne za kibingwa," alisema Dk. Liggyle.

Alisema ujio wa madaktari hao ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuhakikisha huduma zote za kibingwa zinapatikana nchini na kuifanya Tanzania kuwa kituo cha matibabu barani Afrika.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema madaktari hao pia watafundisha wanafunzi.

"Ujio wa wataalamu hawa una tija kubwa kwa MOI na nchi kwa ujumla kwa sababu watafanya upasuaji wa kushirikiana na madaktari bingwa wazalendo jambo ambalo litawezesha kubadilishana uzoefu na kupeana mbinu za kisasa.

"Pia watatoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi kwani moja ya malengo ya MOI ni kutoa mafunzo," alisema Dk. Boniface.

Kwa upande wake, kiongozi wa timu ya madaktari bingwa kutoka China, Dk. Meng Yong, alisema ni heshima kubwa kupata fursa ya kufanya kazi Tanzania.

Alisema wanafuraha kuja kuwahudumia Watanzania kwa kipindi cha miaka miwili na pia watapata nafasi ya kubadilishana uzoefu na madaktari bingwa wenzao wa Tanzania na kujifunza mambo mengi.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka (watatu kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa viongozi wa mgodi wa North Mara alipoutembelea juzi, kuangalia hali ya utunzaji wa mazingira. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wawili washikiliwa tuhuma za mauaji ya mwanamke

**Na Jenifer Gilla**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kula njama na kumuua Barke Pesa Rashid (30), mkazi wa Ilala Utete jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi, Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, ACP Muliro Jumanne, aliwaambia waandishi wa habari jana.

Alisema, Januari mosi, mwaka huu, katika nyumba ya wageni Tabata Segerea, mtuhumiwa wa kwanza Jonsiner Bounser (34), anadaiwa kumuua mpenzi wake baada ya kula njama na mtuhumiwa wa pili aliyefahamika kwa jina la White (33).

"Chanzo cha kifo ni mwanamke huyo kukabwa shingo mpaka kupoteza maisha akiwa katika nyumba hiyo na inadaiwa kuwa mtuhumiwa wa kwanza alikodiwa na mtuhumiwa wa pili kwa malipo ya Sh. 1,700,000 ili amtongoze na baadaye kumuua," alisema Kamanda Muliro.

"Kisa cha mauaji hayo inadaiwa kuwa mtuhumiwa wa pili alimgharamia mwanamke huyo na kumpangishia nyumba, lakini alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengine."

Katika tukio lingine, Muliro alisema wanawashikilia watu sita kwa tuhuma za kuiba vitabu lililotokea Mabibo External, jijini Dar es Salaam, Januari 23, mwaka huu.

Alisema vitabu hivyo vilikuwa kwenye viroba 19 na tayari vilikwishapakiwa kwenye magari yenye namba za usajili T 718 DXW aina ya Pro Box na T 931 DNG aina ya Noah.

"Watuhumiwa hawa wanahojiwa kwa kina na watafikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo. Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam linaendelea kuwashukuru wananchi wema wanaoendelea kutoa taarifa za kweli zinazosaidia kufuatilia na kuwakamata wahalifu kabla au baada ya uhalifu," alisema Muliro.


UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**TENDER NOTICE**

**REQUEST FOR PROPOSAL: No. RFP/2022/SUP/002**
**PROPOSED DESIGN OF THREE STOREY BUILDING, PERIMETER WALL AND GYM FACILITY AT UNHCR KIGOMA SUB OFFICE**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified firms to submit firm offers for provision of consultancy services.

**2. Eligibility:**

Firms duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

Kindly download the tender documents in the below link:

**https://drive.google.com/drive/folders/1dnZ4YO8lZT8XuNTjb83kot-7BmBNQ-oh?usp=sharing**

If you fail to access the link, please write to **ndassa@unhcr.org** copy **ishobeza@unhcr.org**

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Mandatory site visit is scheduled at UNHCR Sub office Kigoma | Thursday 03rd February 2022 at 1100hrs EAT |
| Deadline for receiving requests for clarification | Monday 04th February 2022 at 2359 hrs EAT |
| Deadline for submission of offers | Friday 18th February 2022 at 1600hrs EAT |

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.*



## Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) Publication of Bi-Annual Income and Expenditure.

Lawyers' Environmental Action Team is a Non-Governmental Organization which was founded in 1994 and is registered under the NGOs Act of 2002 with (Certificate of Compliance No. 1985).

Vision: Tanzania with sustainable and well-managed environment and natural resources for current and future generations.
Mission: To contribute towards good governance in the use and sustainable management of the environment and natural resources through public interest litigation, advocacy, strategic research, capacity building, and networking.

In accordance with Non-Governmental Organization (Amendment) Regulation, 2018, Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) is pleased to publish the amount of funds received and expended from July, 2021 to December, 2021.

**Bi-Annual Income and Expenditure for the period from July 2021 to December 2021**

| | |
|---|---|
| **Income:** | **TZS** |
| Receipt from Donors | 985,723,820.87 |
| Bank Interest | 111,655.00 |
| **Total Income** | **985,835,475.87** |
| **Expenditure on:** | |
| Legally empowering Urbanites living in Dar es Salaam to access and enforce a right to live in a clean environment | 80,295,278.91 |
| Examining the Extractive Industry Legal Regime in Tanzania | 31,076,078.98 |
| Usimamizi Endelevu wa Maliasili in Tanzania | 774,418,831.68 |
| Collective Action for Rights Realization in the Extractive Industry | 100,045,286.30 |
| Human & Admin Resources Activities | 25,381,681.52 |
| **Total Expenditure** | **985,835,475.87** |

In sum, LEAT received grants from the following donors: Legal Services Facility (LSF), Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), United States Agency for International Development (USAID-Tanzania); and VSO-Tanzania.

**Lawyers' Environmental Action Team (LEAT),**
**Mazingira House, Mazingira Street, Mikocheni B,**
**House No 8,**
**P.O. Box 12605, Dar es Salaam.**
**Email: info @leat.or.tz.**

# Japan yaisaidia TRA vifaa kuzuia upotevu mapato

Na Maulid Mmbaga

SERIKALI ya Japan kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Japan (JICA), imeipatia Tanzania kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA) msaada wa vifaa mbalimbali yakiwamo magari matatu aina ya Nissan Patrol na boti moja ili visaidie kuzuia vitendo vinavyosababisha upotevu wa mapato.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, alisema magari hayo yatasaidia kuimarisha doria kwenye mikoa ambayo ina biashara za magendo kwa wingi.

Aliitaja mikoa ambayo magari hayo yatapelekwa ikiwamo Dar es Salaam, mpaka wa Kasumulu mkoani Mbeya na Tunduma mkoani Ruvuma pamoja na boti ambayo itakuwa ikifanya doria ya kudhibiti magendo katika Bahari ya Hindi, na kusisitiza kuwapo upotevu wa mapato mengi katika ukanda huo.

"Wote tunafahamu tunapoteza mapato mengi kwenye ukanda wa Bahari ya Hindi, hivyo tumepatiwa boti nzuri inayoenda kasi ambayo itatusaidia kulinda mpaka katika eneo hilo, lakini wametupatia kifaa kinachotumika kukagua mizigo (X-ray baggage scanner).

"Kifaa hicho tayari kimeshasimikwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNIA), kazi kubwa ni kudhibiti mizigo ya mikononi ili kufahamu kilichomo na kuhakikisha mapato ya serikali hayapotei," alisema Kidata.

Pia alisema vifaa vingine vilivyotolewa ni pamoja na vya kugundua dawa za kulevya (Drug detection kits) ambavyo




vitasaidia kuzuia upitishaji wa dawa hizo nchini na (Portable Raman Spectrometer) ambayo ni kwa ajili ya kutambua dawa za kulevya na vilipuzi ndani na nje ya jengo.

Alisema dhumuni la msaada huo ni katika kuhakikisha kwamba (TRA) inapata mapato yake halali na kuzuia uvujaji wa mapato ambao unatokana na biashara za magendo, pia kuhakikisha kwamba afya za Watanzania zinalindwa kwa kuzuia dawa za kulevya.

Kwa upande wake Balozi wa Japan nchini Goto Shinichi, alisema msaada wa vifaa hivyo umelenga kusaidia katika kukuza zaidi maendeleo ya uchumi wa kikanda kupitia uwezeshaji kibiashara na udhibiti salama wa mipaka.

"Hii itasaidia kukuza ushirikiano kati ya Tanzania na Japan, lakini kuchochea maendeleo ya kiuchumi kijamii, kikanda na bara, wakati huo huo, usimamizi mzuri wa mipaka pia utazingatiwa katika kudhibiti wahalifu wa kuvuka mipaka kama vile magendo na kuchukua hatua dhidi ya kuenea kwa COVID-19," alisema Shinichi.

# Kesi ya kujiuzulu Ndugai kuanza leo

Na Kulwa Mzee

JOPO la majaji watatu leo linatarajia kuanza kusikiliza kesi ya kikatiba iliyofunguliwa na Mwenyekiti wa NCCR- Mageuzi, James Mbatia kupinga kujiuzulu kwa aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai na hatua za kupata spika mwingine kwa madai utaratibu ni batili.

Jopo la majaji watatu linaloongozwa na Mwenyekiti Jaji John Mugeta, linatarajia kusikiliza shauri hilo namba mbili la mwaka 2022 lililofunguliwa chini ya hati ya dharura.

Wengine kwenye jopo hilo ni Benhaji Masoud na Jaji Sedekia Kisanya.

Mleta maombi katika kesi hiyo ni Mbatia, wakati mjibu maombi wa kwanza ni Ndugai, wa pili ni Katibu wa Bunge na mdaiwa wa tatu ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Mjibu maombi wa pili na watatu wanawakilishwa na Mawakili Wakuu wa Serikali, Mussa Mbura, Deodatus Nyoni, Andrew Chang'a na Wakili wa Serikali Stanley Kalokola.

Mjibu maombi wa kwanza na wakili wake wanatarajiwa kufika mahakamani kusikiliza shauri hilo ambalo lilikwama kuendelea juzi.

Mahakama ilikataa kutoa siku 14 kwa mawakili wa serikali waliokuwa wameziomba kwa ajili ya kujibu kiapo kinzani badala yake walitakiwa hadi jana saa 8.30 mchana wawe wamewasilisha majibu hayo.

Wakili wa mleta maombi, Mpare Mpoki, alidai dharura katika shauri hilo ipo kwa sababu kuna uchaguzi wa spika.

"Tunachoharakia uchaguzi wa spika usifanyike, busara ya mahakama hii inatakiwa itoke kabla ya uchaguzi wa spika Januari 31, mwaka huu.

" Mahakama pekee ndiyo inayoweza kusimamisha uchaguzi wa spika," alidai Mpoki.

Juzi mahakama iliagiza mjibu maombi wa kwanza Ndugai apelekewe hati ya wito mkononi badala ya email kama ilivyofanyika, kabla ya jana saa 8.30.

Mbatia anapinga utaratibu uliotumiwa na aliyekuwa Spika wa Bunge Job Ndugai kujiuzulu na mchakato wa kupata spika mwingine.

"Katiba imeweka utaratibu, spika akitaka kujiuzulu anatakiwa kwenda kufanya hivyo kwa watu waliomchagua ambao ni wabunge.

"Utaratibu uliotumiwa na Ndugai ni batili haukubaliki kikatiba," alidai Mbatia.

Ndugai alijiuzulu uspika Januari 6 mwaka huu na Januari 21 mwaka huu, Dk. Tulia Ackson aliteuliwa kugombea uspika.




Hallmark Attorneys

NOTICE OF RECEIVERSHIP OF FIFTY (50) UNITS IN UHURU HEIGHTS BUILDING – DAR ES SALAAM

I, Walter Buxton Chipeta, of Hallmark Attorneys of P.O. Box 13811, Dar es Salaam **HEREBY GIVE NOTICE TO THE PUBLIC** that with effect from 17th January 2022, I have been appointed by Exim Bank (Tanzania) Limited of P.O. Box 1431, Dar es Salaam to act as the Receiver /Manager of properties comprised on Plot No. 63/17 with CT No. 38083/4, 38083/10, 38083/11, 38083/17, 38083/18, 38083/23, 38083/31, 38083/32, 38083/33, 38083/36, 38083/38, 38083/89, 38083/127, 38083/128, 38083/129, 38083/131, 38083/133, 38083/134, 38083/135, 38083/136, 38083/137, 38083/138, 38083/161, 38083/162, 38083/176, 38083/180, 38083/198, 38083/201, 38083/204, 38083/205, 38083/206, 38083/207, 38083/208, 38083/209, 38083/210, 38083/211, 38083/212, 38083/213, 38083/214, 38083/215, 38083/216, 38083/217, 38083/218, 38083/219, 38083/220, 38083/221, 38083/222, 38083/223, 38083/224, 38083/225 in the name of **COSMOS PROPERTIES LIMITED** (the Company) of P. O. Box 2205, Dar es Salaam, pursuant to the Mortgage Deed dated 10th November 2010 together with the Deed of First Variation of Mortgage dated 5th March 2012 and two Mortgage Deed dated 28th October 2018.

**TAKE NOTICE THAT** from the date of this notice all transactions involving or in relation to the said properties shall be done through the Receiver/Manager at the address shown herein below.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** any transaction done by the Company or for the Company by any of its Directors or agents, without the express approval of the Receiver/Manager, including any financial transactions or agreements, in respect of the aforementioned properties shall be void and unlawful.

**WALTER BUXTON CHIPETA**
**RECEIVER/MANAGER**
**C/O HALLMARK ATTORNEYS**
**18 RUVU/ CHOLE ROAD,**
**MASAKI AREA**
**P. O. BOX 13811,**
**DAR ES SALAAM.**
**Email: info@hallmarkattorneys.co.tz**
**Tel: +255 22 2601 314/6**

166677



Form 106a

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

**Notice of appointment of receiver or manager**
**Pursuant to Section 106(1) of the Companies Act 2002**

To the Registrar of Companies

Company Number: **60888**

Name of company (Full Name): **COSMOS PROPERTIES LIMITED**

We **EXIM BANK (TANZANIA) LIMITED** of P.O. Box 1431, Dar es Salaam, Tanzania give notice that **WALTER BUXTON CHIPETA** of **HALLMARK ATTORNEYS (name of Firm/Office) PO BOX 13811 DAR ES SALAAM**, Tanzania was appointed as Receiver Manager of the property of the Company with the mandate provided under the Deed of Appointment and the law.

The appointment was made by **EXIM BANK (TANZANIA) LTD** under the powers contained in the **MORTGAGE DEED DATED 10th November 2010** and which was registered on 24th November 2010 **and deed of variation of Mortgage dated 5th March 2012 and DEEDS OF MORTGAGE dated 28th November 2018** which created a charge over the landed properties comprised of Plot No. 63/27 with CT No.38083/4, 38083/10, 38083/11, 38083/17, 38083/18, 38083/23, 38083/31, 38083/32, 38083/33, 38083/36, 38083/38, 38083/89, 38083/127, 38083/128, 38083/129, 38083/131, 38083/133, 38083/134, 38083/135, 38083/136, 38083/137, 38083/138, 38083/161, 38083/162, 38083/176, 38083/180, 38083/198, 38083/201, 38083/204, 38083/205, 38083/206, 38083/207, 38083/208, 38083/209, 38083/210, 38083/211, 38083/212, 38083/213, 38083/214, 38083/215, 38083/216, 38083/217, 38083/218, 38083/219, 38083/220, 38083/221, 38083/222, 38083/223, 38083/224, 38083/225

within the charges in the name of **EXIM BANK (TANZANIA) LIMITED** (a copy of the deed of appointment is annexed).

Name: Edmund Aaron Mnyoga Signature: [signature]
Designation: Head of Legal Date: 17/1/2022 [SEAL]

KINSWAGA [signature]

Designation: CHIEF FINANCE OFFICER

FOR OFFICIAL USE ONLY.

166676

HABARI KITAIFA

# Majaliwa aagiza kufuatiliwa shule zinazotoza michango

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kufuatilia katika maeneo yao ili kuona kama kuna shule zinaendelea kuchangisha michango iliyozuiliwa na serikali.

Pia amewataka wazazi kushirikiana na walimu kuweka mazingira mazuri ya kitaaluma, ili wahakikishe watoto wa kitanzania wanapata elimu bora.

Alitoa maagizo hayo jana alipokagua ujenzi wa madarasa ya Shule ya Sekondari Babati iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara.

"Wazazi lazima tushirikiane na walimu ili kuhakikisha watoto wote waliofikia umri wa kwenda shule wanakwenda na ni marufuku kuwakuta wakifanya biashara. Mtoto lazima asome, "alisema Majaliwa.

Pia Majaliwa alimwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo, Lazaro Twange, asimamie maboresho ya madawati katika shule hiyo kwa kuweka mbao badala ya mabati kama ilivyo sasa.

"...Madawati haya si mazuri yarekebishwe ili kuepusha madhara kwa watoto wetu. Marekebisho haya yanatakiwa yafanyike bila kuathiri mwenendo wa masomo kwa wanafunzi." Alisema.

Katika hatua nyingine, Majaliwa ametumia fursa hiyo kuwaondoa hofu wananchi wote kuhusu gharama za kuunganishiwa umeme vijijini kwamba itaendelea kuwa Sh. 27,000.

Alisema wananchi hususani waishio vijijini hawahusiki na ongezeko la gharama za kuunganishiwa huduma ya umeme iliyotolewa hivi karibuni na Wizara ya Nishati.

## Wakazi Goba walalamika kero dampo kwenye makazi yao

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Mtaa wa Lalata, Kata ya Goba, mkoani Dar es Salaam, wamelalamika kero ya harufu kali ya dampo wanayokumbana nayo mtaani hapo na kuhofia afya zao.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakazi hao walisema juhudi zao za kutatuliwa kero hiyo zimegonga mwamba, licha ya kutoa taarifa kwenye uongozi wa kata.

Nipashe ilipouliza Ofisi ya Mtendaji Mtaa wa Goba, ilikiri suala hilo kuwa la muda mrefu na kwamba limetolewa tangazo kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kuzoa taka hizo na kuzipeleka dampo la Pugu.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Goba, Bakari Mshanga, kupitia tangazo alilolitoa na kuwekwa saini yake, linaonyesha kutangazwa kwa zabuni ya uondoshaji taka ngumu kwenye mtaa huo.

"Watoa huduma wanaotakiwa kupewa zabuni ni wenye leseni ya biashara, uwezo wa vifaa, mtaji, wawe wataalamu wa afya na mazingira na kuzipeleka dampo la Pugu," alisema Mshanga kwenye tangazo hilo.

Alphonce Mbelwa, mkazi wa mtaa huo, alisema suala la kutupwa taka eneo hilo bila ya kuwapo utaratibu wa kuziondoa kila baada ya muda, imekuwa kero kwao kwa muda mrefu.

"Kwa kweli hili suala la utupaji taka mtaa huu sehemu ya Mwanambilimbi, imekuwa kero kwetu maana upepo ukivuma harufu mbaya ya zile taka inasambaa kwenye makazi yetu.

"Hili suala tangu mwaka jana, tumekuwa tukilalamika na kumshirikisha mwenyekiti wa mtaa, lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kudhibiti hiyo hali," alisema Mbelwa.

Gladness Prosper mkazi wa mtaa wa Lalata, alisema yeye ni mwathiriwa mkubwa kwa kuwa anaishi jirani na dampo hilo huku akiishi na harufu ya taka kwa takribani mwaka.

"Yaani mimi madirisha, milango badala ya kuingiza hewa safi napata hewa yenye harufu kali wakati mwingine taka hizi huchomwa, moshi unatoka saa 24, mbaya zaidi hazizolewi.

"Kifusi cha taka za mwaka mmoja fikiria ni tripu ngapi za lori. Ni taka nyingi mno ambazo zitahitaji gharama kubwa kuziondoa licha ya kutoa taarifa serikali ya mtaa mapema.

Alisema, awali baadhi ya wakazi walimtafuta mjumbe wa serikali ya mtaa, na akaahidi kufikisha ujumbe kwa mwenyekiti, ingawa hakuna majibu hadi hivi sasa.

"Nilipoamua kumfuata mwenyekiti na kumueleza akawa anadai kuwa alishawakataza watu wasitupe uchafu, nashangaa kwa nini bado wanaendelea kutupa taka," alisema Gladness.

Alibainisha kwamba, juhudi binafsi za wananchi zilijikita kwa kuyazuia magari ya taka kumwaga, ingawa changamoto ni muda wa usiku ambao wanautumia kufika.

"Sasa swali ninalo jiuliza ni kwa nini hayo magari yamwage taka huku, wakati eneo maalumu la kumwaga taka ni Pugu? Huku wanakuja kufanya nini wakati ni kinyume na taratibu," alihoji Gladness.

Aidha, Nipashe ilipozungumza na Diwani wa Kata ya Goba, Esther Ndoha, alisema anafahamu suala hilo na yupo nje ya Mkoa wa Dar es Salaam na kwamba atalizungumzia atakaporejea.


SERENGETI BREWERIES

18 Januari 2022

## YAH: NAFASI YA USAMBAZAJI BIA NA POMBE KALI

Kampuni ya bia ya Serengeti inatafuta washirika katika usambazaji wa bidhaa zake kwenye mikoa ifuatayo

- Dar es Salaam na Pwani

Kampuni inatafuta wasambazaji wenye ujuzi wa biashara na wenye ari ya kuchochea ukuaji wa biashara yetu ya rejareja na kuongeza wateja.

**Vigezo muhimu ili kuwa msambazaji wetu ni pamoja na;**

1) Ufahamu wa kutosha wa mkoa ikijumuisha ruti, maeneo ya biashara na uwezo wa kutambua maeneo yenye biasahara.
2) Ofisi yenye mtandao (intaneti), printa na kompyuta.
3) Iwe kampuni iliyosajiliwa hapa nchini na iliyokidhi mahitaji yote ya kisheria.
4) Uzoefu katika biashara ya usambazaji itakuwa ni faida ya ziada.
5) Leseni ya biashara.

**Vigezo maalumu kwa msambazaji wa bia:**

1) Mtaji usiopungua TSHs 200,000,000
2) Nafasi ya kutosheleza ghala/stoo itakayowezesha kuhifadhi zisizopungua kreti 10,000.
3) Timu yenye uwezo ya mauzo pamoja na timu ya kutoa msaada zikiwa na msimamiaji wa bidhaa mmoja, watu wanne wa mauzo katika gari ndogo, mtunza fedha mmoja na wapakiaji watano.
4) Magari manne ya usambazaji yenye tani tatu kila moja.

**Vigezo maalumu kwa msambazaji wa pombe kali:**

1) Mtaji usiopungua TSHs 50,000,000
2) Nafasi ya kutosheleza ghala/stoo itakayowezesha kuhifadhi kreti zisizopungua kreti 1,500.
3) Timu yenye uwezo ya mauzo pamoja na timu ya kutoa msaada zikiwa na msimamiaji wa bidhaa mmoja, watu watatu wa mauzo katika gari ndogo.
4) Gari linaloweza kusambaza pombe kali – magari matatu ya wastani wa kati.

Maombi yaambatane na: leseni ya biashara, taarifa ya benki ya miezi 3 (statement), and uthibitisho wa usajili wa biashara BRELA.

Maombi yanaweza kutumwa kwenda: **Anthony.Msanga@diageo.com**

**Au kwenye anuani ifuatayo;**

Kwa: Baraka Kilimba,

Serengeti Breweries Limited,

P.O.Box 41080, Dar es salaam, Tanzania.

Plot 117/2 Access Road, Nelson Mandela Expressway, Chang'ombe.

**Anthony Msanga**
**Meneja Msambazaji**

Johnnie Walker Keep Walking · Smirnoff · Cîroc · Captain Morgan · Baileys · Gordon's ...Shall We? · Bongo Don Spirit · Guinness Made of More · Pilsner Lager · Serengeti Lite · Serengeti

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuna jukumu kumaliza mauaji haya ya kikatili

**MATUKIO** ya mauaji yameshika kasi kwa sasa, kitu ambacho kinaonyesha kwamba kuna tatizo kubwa katika jamii yetu, ambalo linahitaji kupatiwa ufumbuzi.

Matukio kadhaa yamekuwa yakiripotiwa kila uchao na vyombo vya habari na kuthibitishwa na Jeshi la Polisi katika maeneo mengi nchini, huku matukio mengi yakihusisha mauaji ya familia katika mazingira yanayoacha shaka kutokana na wanaofanya vitendo hivyo kutojulikana.

Kwa kutaja baadhi ya matukio hayo

Januari 17, mjamzito na watoto wake wadogo wawili waliuawa kwa kuchinjwa ndani ya nyumba yao na watu wasiojulikana kisha kutokomea.

Lingine lililotokea wiki iliyopita ni la watu watano wa familia moja wakazi wa Kijiji cha Zanka wilayani Bahi mkoani Dodoma kuuawa kikatili na watu wasiojulikana huku miili yao ikikutwa ndani ya nyumba yao ikiwa imeanza kuharibika.

Limo pia la watu watano wakiwamo mke na mume kwa kuhusika na mauaji ya wanandugu watatu waliokutwa wameuawa na miili yao kutupwa mto Jellys eneo la Buzuruga wilayani Ilemela mkoani humo.

Hakika mauaji haya ni ya kushangaza kutokana na kuhusisha watu wengi wa familia moja, kitu ambacho kinamaanisha kuwa si mauaji ya bahati mbaya, bali ni ya makusudi.

Katika hali hii hakuna sababu ya kulitupia mzigo Jeshi la Polisi pekee kutafuta suluhisho, bali jamii nzima inao wajibu wa kujitafakari na kuchukua hatua za kuleta ufumbuzi wa matukio haya.

Kitu cha kwanza ambacho tunapaswa kukifanyia tafakuri ya kina kama taifa, ni kwa nini watu wameondokewa na hofu ya Mungu kutokana na mafundisho ya dini kukataza binadamu kutoa uhai wa binadamu mwenzake. Katazo hilo pia limo kwenye sheria za dola ikiwamo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tunaona kwamba hakuna sababu ya mamlaka zenye jukumu la kushughulikia jamii kama maofisa wa ustawi wa jamii kutokaa ofisini badala yake waende kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na njia sahihi za kutatua migogoro.

Wawahimize kuzitumia mahakama na vyombo vingine kama mabaraza ya ardhi badala ya kujichukulia hatua mkononi, ikiwamo kufanya mauaji, ambayo yana athari mbaya kwa jamii nzima.


Kwa upande wa viongozi wa dini, tunawakumbusha kuendelea kutekeleza wajibu wao wa kuwahubiria na kuwakumbusha wafuasi wao na jamii nzima kutenda matendo mema kama vitabu vitakatifu vinavyoelekeza, hivyo kuwa na hofu na Mungu.

Kadhalika, tunayakumbusha mashirika yasiyo ya kiserikali hususan yanayojihusisha na masuala ya haki za binadamu kijikita kupeleka elimu ya haki za binadamu katika maeneo yote ya nchi hususan vijijini, ambako matukio mengi ya mauaji yanatokea.

Tanzania tuna bahati ya kuwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambayo baadhi ya majukumu yake ni kukemea, kufuatilia matukio mbalimbali ya ukiukwaji wa haki za binadamu ya kutoa mapendekezo ya namna ya kuyashughulikia. Bila shaka tume itakaa kimya kuhusiana na matukio yanayoendelea ya kwamba bado yapo kwenye uchunguzi wa Polisi.

Msisitizo wetu kwa jamii ni kwamba ijenge utamaduni wa kuzitumia mahakama katika kushughulikia migogoro na badala ya kujichukulia sheria mikononi, ikiwamo kufanya vitendo vya mauaji ambavyo vinawaathiri hata watu wengine wasio na hatia hususan watoto.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Dainess Mwakaje, SJMC

## Muungwana Lazima Nilonge

# Malezi mema kwanza, si kudekeza watoto

**BAADHI** ya wazazi na walezi wamekuwa wakichangia kukosekana kwa maadili ya watoto wao kwa kushindwa kuwasimamia na kuwaacha huru huku wakiwadekeza wakifanya wapendalo.

Watoto wapo huru kufanya kile wanachokiona kama ni kutembea usiku, kwenda disko, vibanda umiza na hata ngoma za 'vigodoro' huku wazazi au walezi wakiwaachia hata kama umri hauruhusu.

Suala la maadili ni jambo nyeti ambalo linatakiwa kuzingatiwa na wote, lakini hatua ya kwanza ni kwenye makuzi ya mtoto nyumbani kwenye familia, wazazi na walezi.

Kuna msemo 'mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.' Kwamba ukimkuza katika mienendo mema hawezi kubadilika kwa kuwa tayari umemjengea msingi bora tangu alivyokuwa mdogo.

Imenilazimu kuzungumzia jambo hili kwa kuwa wapo baadhi ya wazazi na walezi hawajali maadili kwa watoto inayozalisha kizazi kisicho na maadili.

Malezi ya aina hiyo, huwaingiza watoto kwenye vitendo viovu katika umri mdogo kwa kuwa wapo huru kufanya wapendavyo.

Nia si kumtafuta mchawi kwani suala la malezi ni jukumu la wote, hivyo kila mmoja awajibike kumkuza mtoto katika malezi bora na yanayokubalika. Ni muhimu kwa wazazi na walezi kutambua makosa wanayoyafanya katika malezi na kujirekebisha.

Cha muhimu ni kumfundisha kuelewa kuwa maisha yanabadilika, awe na maadili, heshima na kumjua Mungu na kumheshimu. Afahamu uaminifu, heshima na kusema ukweli.

Mtoto afahamu kuwa kuna wakati unaweza kuwa nacho na siku nyingine huna hivyo ni vyema, ajue kukabiliana na hali zote iwe kupata au kukosa kuliko kumtimizia kila anachohitaji hata kama hauna uwezo wakati huo.

Aidha, kumsifia mtoto kwa kila jambo bila kumpinga ni hatari kwa malezi kwa vile watoto wana tabia ya kukariri mambo hivyo mzazi au mlezi wawe makini kuwakosoa si tu kuwasifia au kuwaunga mkono kwa kila wanalofanya.

Pia kutokutoa ushirikiano unapopata taarifa mbaya kumhusu mtoto ni kosa linalofanywa na wazazi au walezi hasa zinapohusu matendo mabaya, wengi wanawatetea hata kama kuna ushahidi.

Hali hii husababisha watoto wengi kuendeleza mienendo mibovu, kama udokozi, wizi na utukutu. Hivyo ni muhimu kwa wazazi kutoa ushirikiano wanapokea habari za mienendo mibaya ya watoto wao.

Kutumia lugha chafu wakati wa mazungumzo ni kosa linalofanywa na wazazi au walezi wanapozungumza wao kwa wao au wanapoongea na mtoto.

Si vizuri kuongea matusi au maneno yasiyofaa mbele ya mtoto kwani hukariri lugha au maneno kama hayo na kuyatumia pia katika mazungumzo yao.

Kuandaa mazingira yasiyomjenga mtoto kukua katika malezi bora. Katika kujadili suala la malezi pia mwanasaikolojia Duee Wilson anasema: "Mtoto anaweza kuchukua tabia nzuri au mbaya hata kabla hajazaliwa, kwa mfano kuwa na tabia za chuki kutokana na baba na mama kutokuelewana."

Aina ya malezi mzazi au mlezi anayomjengea mtoto, kama tabia zisizofaa hutegemea na mazingira, wanaowazunguka, muda wanaotumia katika maisha ya kila siku.

Lakini tabia zinaweza kusababishwa na aina nne za malezi mojawapo ni malezi ambayo mtoto na wazazi au walezi wanakua na mahusiano chanya.

Uhusiano kati ya mzazi na mtoto unakuwa mbaya mfano ukali na adhabu kali apewazo, utii unapewa kipaumbele zaidi, sheria zinazowekwa na wazazi au walezi zinakuwa hazitolewi maelezo, lakini mtoto hasikilizwi. Hivyo ni vyema kuweka mizani na kuhakikisha mtoto ananyooka.

**HABARI KITAIFA**

## Wananchi Mpanda kuanza kunufaika kwa mikopo ya TCB

**Na Christina Mwakangale**

WANANCHI wa Wilaya ya Mpanda, mkoani Katavi, wataanza kunufaika na mikopo kutoka Benki ya Biashara Tanzania (TCB), baada ya kufungua tawi mkoani humo.

Mkurugenzi Mtendaji TCB, Sabasaba Moshingi, aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa tawi hilo, lililozinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko.

Moshingi alisema benki hiyo ni kati ya zenye mtandao mpana wa matawi unaojumuisha matawi makubwa 47 na madogo 35 nchini, na kwamba wigo wa huduma za kibenki unawahusisha mawakala zaidi ya 3,800. "Tawi jipya la Mpanda, litarahisisha utoaji huduma za kibenki mkoani Katavi na kuwapunguzia wananchi safari za kuzifuata huduma mbali na makazi yao na sehemu wanazofanyia kazi.

"Kufunguliwa kwa tawi hili la Mpanda kumezingatia shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa wilayani humu kupitia wafanyabiashara, wafugaji na wakulima pamoja na fursa zilizopo," alisema Moshingi.

Alibainisha kwamba, ili kukuza wigo wa shughuli za kiuchumi, wananchi watanufaika na huduma mbalimbali zikiwamo za mikopo, inayotolewa na benki hiyo, kuanzia shilingi 500,000 na kuendelea kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao ya kifedha.

Moshingi aliongeza kwamba, benki hiyo imejikita katika kuhakikisha huduma nafuu za kibenki zinapatikana kwa urahisi , hasusan vijijini ambako Watanzania wengi wanaishi.

"TCB sio kwamba tu ni benki kubwa nchini, bali pia inatoa mchango mkubwa katika shughuli za kijamii hasa kuinua viwango vya elimu pamoja na upatikanaji wa huduma bora za afya," alisisitiza.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mrindoko, aliipongeza benki hiyo kwa uwekezaji huo, akisema utakuwa wa manufaa kiuchumi na kifedha na kwamba umekuja wakati muafaka,

"Huduma za kibenki zinahitajika mkoani humu kwa muda mrefu sasa, uwepo wa tawi hili kutaongeza idadi ya wananchi wenye akaunti za benki kitu ambacho ni muhimu kwenye maendeleo ya huduma jumuishi za fedha na shughuli za uzalishaji kwa ujumla," alisema Mrindoko.

"Katavi ni mkoa tajiri uliojaliwa rasilimali nyingi kwa hiyo uwepo wa huduma za kibenki za uhakika ni suala muhimu sana kwa ajili ya maendeleo."

## Machinjio sasa kuanza uchinjaji ng'ombe 100, mbuzi 1,000 kila siku

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MACHINJIO ya kisasa ya mifugo ya Nguru Hills Ranch Ltd yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku yaliyoko wilayani Mvomero Mkoa wa Morogoro yanatarajiwa kuanza rasmi Machi mosi, mwaka huu, hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na ajira.

Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma (PSSSF ), Fortunatus Magambo, alibainisha hayo kwa wahariri kutoka vyombo vya habari waliofanya ziara ya kutembelea na kujionea maendeleo ya mradi wa machinjio ya kisasa.

Alisema mradi huo wa machinjio hayo unamilikiwa kwa ubia kati ya Serikali kupitia Mfuko wa PSSSF , Eclipse Investiment (LLC) na Kampuni ya Busara Investiment (LLP).

Alisema mradi huo ulianza mwaka 2018, lakini ugonjwa wa Covid -19 ulipoanza ulisababisha mashine zilizoagizwa kutoka nje kuchelewa kuletwa pamoja na wataalamu wake hadi Julai mwaka jana zilipoletwa na kuanza kufungwa na kwamba kazi hiyo ipo kwenye hatua ya mwisho.

Naye Meneja Uhusiano na Elimu kwa wanachama PSSF, James Mlowe, alivitaka vyombo vya habari kuungانisha jamii, Serikali na wadau wa maendeleo katika utoaji wa taarifa sahihi katika uhamasishaji wa kukuza uchumi na maendeleo ya watu.

Mlowe alisema kuwa mfumo wa PSSF umewekeza katika kiwanda hicho wa asilimia 30,ikiwa ni sehemu ya mkakati wake katika uwekezaji wa miradi mbalimbali hasa katika kipindi hiki ambacho taifa limejiwekeza katika uchumi wa viwanda.

# Jaji Kiongozi akemea mauaji ya kikatili

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu Tanzania, Mustafa Siyani, amesema ni aibu wananchi kufanya mauaji ya kikatili, badala ya kutumia mahakama ili kupata haki zao na kuepusha migogoro inayosababisha vifo.

Pia amewataka mahakimu kuacha kujifungia ofisini, badala yake wasikilize kero za jamii ambazo zinasababisha ugomvi na vifo.

Kauli hiyo imetolewa baada ya mauaji ya watu watano wa familia moja yaliyotokea hivi karibuni wilayani Bahi, mkoani Dodoma.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mahakama ya Wilaya ya Chemba, Jaji Kiongozi Siyani alisema watu wemekuwa wakijichukulia sheria mkononi, jambo linalochangia matukio mengi ya mauaji nchini.

"Ni aibu kubwa kuona mauaji kama yale na kuna mahakama, kwanini wasitumie mahakama kutoa malalamiko yao ili wasikilizwe," alisema Jaji Siyani.

Alisema kuwa siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio mengi ya mauaji yanayosababishwa na wananchi kujichukulia sheria mkononi. Miongoni mwa mauaji hayo ni yaliyotokea katika Kijiji cha Zanka Wilaya ya Bahi ambapo watu watano wa familia moja waliuawa. Tukio lingine la wiki iliyopita ni la mauaji ya mjamzito na watoto wake wadogo mkoani Katavi.

"Ni aibu kwa wananchi kutotumia Mahakama kwa kuchukua sheria mikononi, acheni kujichukulia sheria mkononi amani tuliyonayo ndiyo tunu yetu," alisema Jaji Kiongozi.

Aliwataka wananchi wanapokuwa na migogoro watumie mahakama zinazojengwa kila kona nchini, ambapo alisema uwapo wa Mahakama katika Wilaya ya Chemba utawafanya wananchi wapate huduma karibu tofauti na awali walipolazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 40, ili kupata huduma katika Wilaya ya Kondoa.

Alisema Mahakama Tanzania inaendelea na ujenzi na maboresho katika mahakama zake mbalimbali nchini.

Naye Mkuu wa Wilaya alimshukuru Jaji na kumpongeza kutokana na kuleta mahakama eneo hilo, jambo litakalosaidia kupunguza migogoro na watu kupata haki zao za msingi.


A PRODUCT OF The Coca-Cola Company

KILIMANJARO DRINKING WATER

TAARIFA KWA UMMA

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water | kilimanjarodrinkingwater | kdw@bbl.co.tz

+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

# Shaka awakingia kifua Rais Samia, Mwinyi

**Na Beatrice Shayo,** ALIYEKUWA PEMBA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema utekelezaji wa kazi za serikali zitokanazo na matakwa ya ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020/2025 chini ya Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi ni mkakati na matakwa ya sera za chama wala si utashi binafsi.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, wakati akikagua ujenzi wa tawi la CCM liliioko Shehia ya Chimba, Wilaya ya Micheweni, mkoa wa Kaskazini Pemba.

Aidha, alisema wapo baadhi ya watu wanadhani utekelezaji huo unatokana na utashi binafsi huku wakiamini ni makosa yasiyo na umakini na uzalendo. Kiongozi huyo aliwataka wanachama wote kuelewa wana jukumu moja la kulindana, kuteteana na kubaki wamoja nyakati zote za kipupwe, kiangazi na masika.

Alisema marais hao wawili wataendelea kujituma kutokana na utekelezaji wa sera za CCM, na Ilani ya Uchaguzi kwa niaba ya wananchi huku wakitaraji kupata tija na manufaa yatakayokuza tunu, maslahi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

"Watanzania wanatakiwa kujua ushindani wa kisiasa hususan chini ya mfumo wa vyama vingi, kusakamwa na hila na mbinu batili zikilenga kuwagawa, kuwagombanisha wanachama na viongozi wa CCM hatimaye maadui wapate urahisi kuyafikia malengo yao," alisisitiza Shaka.

"Wana CCM wenzangu chonde chonde tambueni utekelezaji wa kisera hufanyika kwa matakwa ya ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020/2025. Rais Samia na mwenzake Dk. Hussein Ali Mwinyi hutekeleza kazi zao kutokana na matakwa ya chama si utashi binafsi," alisema Shaka.

Aliwahimiza wanachama kutokubali kulishwa uzushi na kujikuta wakigawanyika kifikra na kimawazo kwani upinzani unakusudia CCM kuwaondolea ari ya mshikamano wao, umoja na upendo, waendelee kushikamana.

"Watajitokeza maadui aidha ndani au nje ya chama wakidai yanayofanyika sio malengo ya sera bali utashi wa binafsi. Maneno hayo sio kweli, mkae mkijua huo ni uongo, uzushi na upotoshaji. Ni wajibu wetu kushikamana, kupendana, kufanyakazi pamoja usiku na mchana," alisema.

Kwa mujibu wa Shaka, tangu Rais Samia ashike madaraka hapumziki badala yake amekuwa akisafiri ndani na nje akipigania, kutafuta maslahi ya kimaendeleo kwa wananchi wake.

"Wote sisi ni mashahidi kutokana na uchapakazi wa Rais wetu. Kutokana na juhudi zake na uzalendo alionao na mafanikio ya kisera yaliyopatikana chini ya serikali ya awamu ya sita, yametupatia tija na ufanisi wa mfano katika muda wa miezi tisa akiwa madarakani," alisema.

Kwa upande wa Zanzibar, alisema tangu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Mwinyi, kila mmoja amemshuhudia kiongozi huyo anavyohangaika, akijituma na SMZ ikizidi kuvutia wawekezaji kwa lengo la kukuza mkakati wa kujenga uchumi imara na maendeleo ya nchi.


**Canara Bank (Tanzania) Ltd.**

*(Together we can build a better life)*

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2021.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2021 | Robo Mwaka iliopita 30 Septemba 2021 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 832.82 | 548.59 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 9,467.90 | 8,250.04 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 35,070.14 | 33,247.64 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 529.37 | 427.88 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 141.50 | 51.11 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 36,356.91 | 30,126.83 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 51,106.26 | 51,812.46 |
| | 12 Mali Nyingine | 1,071.54 | 1,242.74 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 726.58 | 827.23 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **135,303.03** | **126,534.53** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 36,430.00 | 31,965.00 |
| | 18 Amana za Wateja | 56,595.88 | 52,011.51 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 Amana Maalumu | - | - |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,533.31 | 1,119.31 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipw | - | - |
| | 27 Dhima Nyingine | 493.70 | 1,820.83 |
| | 28 Madeni | - | - |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **95,052.89** | **86,916.65** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **40,250.14** | **39,617.88** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 1,279.37 | 573.03 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 3,516.20 | 4,222.54 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,624.57 | 1,992.32 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,250.14** | **39,617.88** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 6,760.70 | 10,086.28 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 1,632.81 | 1,371.47 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 447.05 | 451.87 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 29.75% | 31.31% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.17% | 2.63% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 55.39% | 62.21% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 37.77% | 40.95% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 90.95% | 91.37% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | 10.78% | -2.49% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | 6.93% | -0.58% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2021 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 31 Desemba 2020 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Desemba 2021 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Desemba 2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,434.39 | 2,425.25 | 9,635.81 | 8,750.58 |
| 2 Gharama za Riba | 805.96 | 864.59 | 3,237.67 | 3,292.98 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,628.43** | **1,560.66** | **6,398.15** | **5,457.60** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (4.82) | 86.49 | 82.90 | 26.23 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **379.58** | **401.26** | **955.34** | **850.83** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 54.75 | 39.23 | 152.73 | 174.73 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 324.83 | 362.02 | 802.60 | 676.10 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **1,025.57** | **962.66** | **3,481.01** | **3,499.44** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 342.02 | 331.84 | 1,376.29 | 1,295.53 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 12.49 | 11.52 | 33.92 | 28.99 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 671.06 | 619.30 | 2,070.80 | 2,174.92 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **987.26** | **912.76** | **3,789.57** | **2,782.76** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 355.00 | 330.00 | 1,165.00 | 840.00 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **632.26** | **582.76** | **2,624.57** | **1,942.76** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 25 | 25 | 25 | 25 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 19 | 18 | 80 | 59 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 19 | 18 | 80 | 59 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.92% | 1.96% | 2.10% | 1.71% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 6.31% | 6.17% | 6.73% | 5.25% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 51.07% | 49.07% | 47.34% | 55.47% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.40% | 5.60% | 5.52% | 5.27% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba | Robo Mwaka iliopita 30 Septemba 2021 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Desemba 2021 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Desemba 2020 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 632.26 | 856.29 | 2,624.57 | 1,942.76 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 100.65 | 100.65 | 402.48 | 451.00 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | 706.20 | (3,332.23) | (2,681.41) | (12,965.86) |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | 9,049.37 | (2,147.57) | 11,776.98 | 11,349.44 |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (492.20) | 890.42 | 753.04 | 1,518.24 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 1,841.94 | (75.92) | 759.87 | (985.29) |
| Kodi iliyolipwa | (355.00) | (270.00) | (1,165.00) | (840.00) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **11,483.22** | **(3,978.36)** | **12,470.54** | **470.30** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | - | (0.69) | (6.03) | (17.86) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 165.85 | 489.89 | (2,005.73) | (11,675.90) |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **165.85** | **489.20** | **(2,011.76)** | **(11,693.75)** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (65.91) | (64.30) | (254.15) | (249.37) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(65.91)** | **(64.30)** | **(254.15)** | **(249.37)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 11,583.16 | (3,553.46) | 10,204.63 | (11,472.82) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 35,518.30 | 39,071.76 | 36,896.83 | 48,369.87 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **47,101.46** | **35,518.30** | **47,101.46** | **36,897.05** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 31/12/2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **4,754.21** | **41.35** | **-** | **-** | **37,625.56** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,624.57 | - | - | - | **2,624.57** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,238.02) | 1,238.02 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **6,140.77** | **1,279.37** | **-** | **-** | **40,250.14** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **2,308.69** | **828.58** | **-** | **-** | **35,967.28** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,658.29 | - | - | - | **1,658.29** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 787.23 | (787.23) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **4,754.21** | **41.35** | **-** | **-** | **37,625.56** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 Desemba 2021

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 21-01-2022 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 21-01-2022 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 21-01-2022 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| RAJAB S KAKUSA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 21-01-2022 |
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 21-01-2022 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 21-01-2022 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**


# Licha ya corona Mo Dewji azidi kung'ara orodha ya mabilionea

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya mlipuko wa virusi vya corona, mabilionea wa Afrika wameongeza utajiri wao kulinganishwa na miaka minane iliyopita, mfanyabiashara maarufu nchini, Mohammed Dewji 'Mo', akiwa miongoni mwa mabilionea 18 barani waliopenya kwenye orodha mpya ya Jarida la Forbes. Kwa mujibu wa ripoti ya jarida hilo iliyotolewa juzi, mabilionea hao wa Bara la Afrika wana utajiri unaokadiriwa kufikia Dola za Marekani bilioni 84.9 ikiwa ni asilimia 15 zaidi ya miezi 12 iliyopita na ongezeko la juu zaidi tangu mwaka 2014 wakati bara lilipokuwa na mabilionea 28 waliokuwa na utajiri wa jumla ya Dola bilioni 96.5.

Katika utafiti wake, Forbes imeripoti kuwa ilitumia vigezo vya akiba ya mali na viwango vya kubadilisha fedha kwa Januari 19, mwaka huu kupima thamani ya utajiri wa mabilionea hao.

Kwa mujibu wa Forbes, mabilionea 18 waliopenya kwenye orodha hiyo wametoka kwenye nchi saba, Afrika Kusini na Misri zikiongoza kwa kuingiza watano kila moja, zikifuatiwa na Nigeria yenye mabilionea watatu.

Kwenye orodha hiyo, Mtanzania Mo Dewji amefungana na Othman Benjelloun (Morocco) na Yousef Mansour (Misri) katika nafasi ya 15, wote wakiwa na utajiri wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.5 kila mmoja.

Katika ripoti yake hiyo, Forbes imebainisha kuwa imezingatia utajiri wa mabilionea wanaoishi Afrika au ambao biashara zao zina mzizi na zinafanyika ndani ya bara hilo.

Kwa kuzingatia kigezo hicho, ripoti mpya ya Forbes imewaweka nje ya orodha mzaliwa wa Sudan Mo Ibrahim, aliyechukua uraia wa Uingereza na mzaliwa wa Misri Mohamed Al-Fayed anayeishi London. Hata hivyo raia wa Zimbabwe Strive Masiyiwa, anayeishi London, amepenya kwenye orodha kwa sababu ya uwekezaji wake katika masuala ya mawasiliano barani Afrika. Ripoti ya Forbes imebainisha kuwa mabilionea wawili kati ya 18 wameporomoka kiutajiri kulinganishwa na mwaka uliopita. Hao ni Mo Dewji wa Tanzania na Koos Bekker wa Afrika Kusini.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, utajiri wa Mo Dewji umeshuka hadi Dola bilioni 1.5 kutoka Dola bilioni 1.6 mwaka mmoja uliopita kutokana na ushindani wa kibiashara wakati Bekker akiporomoka hadi Dola bilioni 2.7 kutoka Dola bilioni 2.8 kutoka na hisa za wabia wake katika masuala ya biashara ya mawasiliano ya intaneti, Naspers na Prosus kupungua kwa zaidi ya asilimia 20 kwa kila mbia.

Ripoti ya Forbes imebainisha kuwa kwa miaka 11 mfululizo sasa, Aliko Dangote wa Nigeria ameendelea kuwa tajiri namba moja barani Afrika, akiwa na utajiri unaokadiriwa kufikia Dola za Marekani bilioni 13.9, akipanda kutoka Dola bilioni 12.1 mwaka jana, sababu kuu ikiwa ni kuongezeka kwa asilimia 30 kwa mauzo ya saruji ya Dangote ambayo ndiyo uwekezaji wake mkubwa zaidi.

"Mabilionea wote barani Afrika ni wanaume, mwanamke wa kwanza kupenya kwenye orodha, Isabel dos Santos wa Angola, alianguka kwenye ripoti ya Forbes ya Januari 2021," ripoti inahitimisha.

## Kizimbani kwa tuhuma za kutakatisha Dola 225,600

**Na Hellen Mwango**

MKAZI wa Ukonga jijini Dar es Salaam, Paul Msoka (47), amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka sita yakiwamo manne ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Dola za Kimarekani 225,600.

Mshtakiwa huyo ambaye ni mfanyabiashara alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Jackline Nyantori, alidai kuwa, Aprili 24, 2021, jijini Dar es Salaam alighushi nyaraka ya Kampuni ya ACGB International Trade, LLC, United State of America (USA), zimeingia katika mkataba na Kampuni ya Tanganyika Mining Company Ltd, kampuni ya kitanzania itauza kilo 20 ya madini ya dhahabu na kusafirisha kwenda San Diego, California, Marekani wakati akijua si kweli.

Shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Desemba 13, 2021 eneo lisilofahamika Dar es Salaam, kwa nia ovu, alighushi akionyesha kwamba cheti kilichoonyesha kwamba Baraza la Taifa la Biashara, Viwanda na Kilimo kwamba limepitisha boksi lenye kilo 20 za madini ya dhahabu kwa ajili ya kusafirisha na Kampuni ya Tanganyika Mining Company Ltd na imethibitishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakati akijua si kweli.

Upande wa Jamhuri uliendelea kudai kuwa siku ya tukio la pili, mshtakiwa pia alighushi hati ya kubadili umiliki ya Desemba 13, akionyesha Southern African Development Community (SADC), ilitoa mabadiliko ya umiliki wa hati hiyo kuruhusu Kampuni ya Tanganyika Mining Company Ltd kusafirisha kilo 20 ya madini ya dhahabu na zisafirishwe kwenda ACGB International Trade iliyoko San Marcos, Marekani wakati akijua si kweli. Katika shtaka la nne ilidaiwa kuwa Desemba 8, 2021 mshtakiwa huyo alighushi nyaraka zilizoonyesha kwamba zimetolewa na Baraza la Usimamizi wa Amani la Umoja wa Mataifa katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (MONUSCO) na kwamba zilizotolewa kwa Kampuni ya Tanganyika Mining Company Ltd ya Tanzania kuiruhusu kampuni hiyo kusafirisha kilo 20 za dhahabu kutoka Kongo kwenda kwa Kampuni ya ACGB International Trade ya Marekani huku akijua si kweli.

Ilidaiwa kuwa, kati ya Juni Mosi, 2021 na Januari 11, 2022 kwa njia ya udanganyifu alijipatia kutoka kwa Aldo Costa ambaye ni mwakilishi wa ACGB International Trade, LLC, Kampuni ya Marekani Dola 225,600 akidanganya kwamba angesambaza kilo 20 ya dhahabu kwa Kampuni ya ACGB wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la utakatishaji, mshtakiwa huyo alidai katika tarehe hizo, mshtakiwa huyo alijipatia kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Aldo Costa huku akijua fedha hizo ni mazalia ya makosa tangulizi ya kughushi.

Mashtaka hakutakiwa kujibu chochote, upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

# Mchungaji aelekeza waumini chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

WAUMINI wa Kanisa la Upendo, wamehimizwa kuzingatia maelekezo ya serikali kuhusu chanjo ya UVIKO-19 kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa afya zao.

Wito huo ulitolewa na Mchungaji Emmanuel Mathias, wakati wa uzinduzi wa kanisa hilo jipya, Mwenge mkoani Dar es Salaam juzi. Alisema serikali imetangaza kuwa chanjo ni hiari, na kwamba kila mtu aangalie umuhimu wa kulinda afya yake, kwa kuwa hakuna anayemlazimisha bali ni kuangalia uwezekano wa kukinga na ugonjwa huo.

"Kanisa letu linaitwa Kanisa la Upendo, tunapendana, hivyo hatuna budi kuelekezana kwa Mungu na pia kuzingatia kile ambacho serikali inatuelekeza kuhusu suala zima la chanjo ya corona," alisema Mchungaji Mathias.

Alisema wataalamu wa afya wameshatoa maelekezo yote ya kujikinga na ugonjwa huo, ikiwamo kuvaa barakoa, kunawa maji tiririka na kutumia vitakasa mikono na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

"Serikali inaelekeza kuwa suala la chanjo ni la hiari, lakini si vibaya sisi wenyewe kujiongeza kwa kuchukua hatua badala ya kukaa kimya tu eti kwa sababu serikali imetangaza kuwa chanjo ni hiari," alisema.

Mchungaji huyo alisema, jamii inapozingatia mwongozo wa udhibiti wa ugonjwa huo kupitia afua ya kudhibiti misongamano katika jamii bila kuathiri shughuli za kiuchumi, waumini hawawezi kujitenga nao.

"Kwa wito wangu ni kwamba, serikali inasema chanjo ni hiari, lakini tunaweza kujiongeza bila kusubiri hiari, ili kulinda afya zetu dhidi ya corona, kwani nchi yetu haiko katika kisiwa kisicho na mwingiliano wa watu," alisema.

Alisema, viongozi wa dini wana sehemu yao katika kuhimiza waumini kuzingatia maelekezo ya muhimu kama hayo, ili waendelee kumtumikia Mungu na kufanya shughuli zao za kila siku wakiwa njema.



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua tawi la Benki ya Biashara Tanzania (TCB), wilayani Mpanda juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi wapewa siri kuepuka kucheleweshewa mafao ya kustaafu

**Na Joseph Mwendapole**

WATUMISHI wa umma wameshauriwa kuhakiki taarifa zao mara kwa mara kabla ya kustaafu ili kuepuka usumbufu wa kucheleweshewa mafao wanapomaliza muda wa utumishi.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro na Kaimu Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Ramadhani Mkeyenge.

Alikuwa akizungumza kwenye kongamano la siku moja na wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) kuhusu hali ya mfuko huo na mafao ya mfuko huo ambao mwaka huu umetimiza miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018.

Mkeyenge alisema tatizo la mkanganyiko wa taarifa za wanachama limekuwa changamoto kubwa hali ambayo inasababisha usumbufu kwa wanachama wengi pale wanapostaafu.

"Ni vizuri mwanachama anapokaribia kustaafu ahakikishe miezi sita kabla anakaa na mwajiri wake kuweka taarifa zake sawa ili akistaafu asisumbuke kurekebisha taarifa hizo na kwa kweli mkanganyiko wa taarifa za mwanachama imekuwa changamoto kubwa sana kwenye malipo," alisema Mkeyenge. Alisema changamoto inayoukabili mfuko ni jamii kukosa elimu kuhusu umuhimu wa hifadhi ya jamii, hivyo PSSSF inajitahidi kutoa elimu kupitia makongamano, matamasha na vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii.

Alisema mfuko umeanzisha mfumo wa kupokea michango ya wanachama kwa njia rahisi ya GePG na kuwapatia wanachama taarifa kuhusu michango yao na kuwapa elimu.

Alisema huduma za mfuko huo kwa sasa zinapatikana kupitia mtandao wa ofisi ulioko nchi nzima katika ngazi ya mikoa kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mkeyenge alisema wameboresha utunzaji wa kumbukumbu za wanachama kwa kutumia mifumo ya kielektroniki na kwamba malipo ya mafao kwa kutumia mifumo ya TEHAMA iliyotengenezwa na wataalamu wa ndani.

Alisema hivi sasa wanalipa mafao moja kwa moja kwa wanufaika kwa njia ya kimtandao (online payments) na wanachama wamekuwa wakihudumiwa kwa njia ya simu ya bure kupitia kituo cha simu ya huduma kwa wateja (Call Center).

Alisema hadi Novemba mwaka jana mfuko ulikuwa umelipa mafao kwa wanachama na wategemezi yanayofikia Sh. bilioni 6.4 ambapo Sh. bilioni 3.3 zililipwa kwa wastaafu na Sh. bilioni 178 zililipwa kwa wategemezi.

Alisema Sh. bilioni 6.45 zililipwa kama fao la kukosa ajira ambayo yalianza kulipwa kuanzia Februari mwaka 2019 na kwamba hadi Novemba mwaka jana mfuko ulisajili wanachama wapya 52,072.

Alisema jumla ya wanachama wachangiaji wa mfuko huo hadi sasa ni 711, 706 na kwamba asilimia 59 ya wanachama wa mfuko huo ni wanaume na asilimia 41 ni wanawake wakati asilimia 78 ya wanachama wote wakiwa chini ya miaka 50.

# Majaliwa awapa wanafunzi malengo kupata maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka watoto wa Kitanzania kujiwekea malengo ya kusoma kwa bidii ili wapate maarifa yatakayolisaidia taifa kupata maendeleo.

Majaliwa alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameiagiza Wizara ya Elimu kufanya mapitio ya sera ili kuifanya sekta hiyo kuendelea kufanya vizuri zaidi.

Alisema hayo juzi alipokagua ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari za Gehandu na Nowu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara.

Alisema kuwa serikali kwa upande wake imejipanga ipasavyo na itaendelea kuweka mazingira bora ya kujifunza na kufundishia ili kuwawezesha kufikia malengo hayo.

Ujenzi wa madarasa hayo unatokana na fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. "Vijana someni hadi mfike chuo kikuu."

Pia Waziri Mkuu ameziagiza halmashauri zote ziweke mpango wa ujenzi wa mabweni kupitia mapato yao ya ndani ili wanafunzi wakae shuleni na kupata muda wa kutosha wa kujisomea. Kadhalika, amewakumbusha watumishi wa umma kutambua kuwa wanajukumu kubwa la kuwatumikia Watanzania na kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Awali, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Gehandu, Mwalimu Gadiel Bei, alimshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha za ujenzi wa vyumba hivyo viwili vya madarasa.

Alisema mbali na madarasa hayo pia wamejenga mengine matano kati yake mawili yametokana na fedha za ruzuku ya EP4R na matatu ni nguvu za wananchi na halmashauri.

Mwalimu Bei alisema kukamilika kwa madarasa hayo kutaiwezesha shule hiyo yenye wanafunzi 945 wa kidato cha kwanza hadi cha sita kuongeza tahasusi nyingine ya kidato cha tano kuanzia mwezi Julai 2022.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Innocent Rwetabura, akizungumza wakati Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kulia), alipofanya ziara ya kikazi katika makao makuu ya kampuni hiyo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Washindi Tuzo ya Kiswahili kutangazwa Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wa mwaka 2022 wa Tuzo ya Kiswahili ya Mabati-Cornell ya Fasihi ya Afrika wanatarajia kutangazwa kesho mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa ALAF Limited, Hawa Bayumi, alisema tuzo hii iliainishwa mwaka 2014.

"Shughuli ya kuwatangaza washindi itafanyika katika ukumbi wa Mlimani City kuanzia asubuhi na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa Fasihi na Lugha ya Kiswahili," alisema na kuongeza kuwa jopo la majaji watatu watasoma baadhi ya kazi bora zilizoshindanishwa na baadaye kutangaza washindi wa jumla katika kila kipengele.

Aliongeza kuwa Tuzo ya Kiswahili ya Mabati-Cornell ya Fasihi ya Kiafrika, yenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani 15,000, hutolewa kila mwaka kwa miswada bora, au kwa vitabu vilivyochapishwa miaka miwili kabla ya mwaka wa kutolewa zawadi, katika fani za riwaya, ushairi, wasifu na riwaya za picha.

Miswada inayoshinda huchapishwa na Shirika la uchapishaji vitabu la East African Educational Publishers (EAEP). Na mswaada bora wa ushairi hufasiriwa kwa Kiingereza na kuchapishwa kitabu na Shirika la Africa Poetry Book Fund.

Madhumuni makuu ya tuzo hii, iliyoanzishwa mwaka 2014 na Dk. Lizzy Attree (Mkurugenzi wa Tuzo ya Caine) na Dk. Mukoma wa Ngugi (Chuo Kikuu cha Cornell, Marekani), ni kuthamini uandishi kwa lugha za Kiafrika, kuhimiza sanaa ya tafsiri baina ya lugha za Kiafrika zenyewe kwa zenyewe, na pia kutafsiri maandishi ya lugha nyingine kwa lugha za Kiafrika.

Tuzo hii inadhaminiwa na kampuni ya ALAF Limited, Tanzania na Mabati Rolling Mills, Kenya (ambazo ni miongoni mwa kampuni za Safal Mauritius Limited); pia na Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa Masuala ya Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Cornell, na Idara ya Taaluma za Afrika ya Chuo Kikuu cha Cornell, Marekani.

# TAMWA yapewa tano kwa kuelimisha jamii

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda, amekipongeza Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), kwa kutoa elimu kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mtanda aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria yenye kauli mbiu 'Zama za Mapinduzi ya nne ya Viwanda, Safari ya Maboresho kuelekea Mahakama Mtandao' uliloshirikisha wadau mbalimbali wa sheria kikiwamo TAMWA.

Mwanachama wa TAMWA, Ashura Mohamed, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa chama hicho, Rose Reuben, kwenye maadhimisho hayo, alisema kuwa TAMWA wako mstari wa mbele katika kutetea wanawake na watoto na kwamba wameshiriki Wiki ya Mahakama kwa lengo la kuelezea mamlaka husika namna wanawake na watoto wanavyofanyiwa ukatili .

"TAMWA tutaendelea kupaza sauti ili kudhibiti ukatili kwa wanawake na watoto kupitia wiki hiyo ya sheria na lengo letu ni kuona vitendo vya ukatili vimekoma," alisema Ashura.

Naye Mkurugenzi wa TAMWA, Rose Ruben, alisema kuwa chama hicho kitaendelea kupaza sauti ili kudhibiti ukatili wa wanawake na watoto kupitia Wiki ya Sheria na kuendelea kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Katika mkutano huu tunawakilishwa na wanachama wetu walioko mkoa wa Arusha, tunamia wanachama wetu wakili Mary Mwita, ambaye anatoa msaada wa kisheria, pamoja na wenzake wanaoandika masuala mbalimbali yenye mrengo wa masuala ya kijinsia, haki za wanawake, wasichana na watoto,"alisema.

Alisema kuwa amepokea pongezi kutoka kwa mkuu wa mkoa na kuwa hii inaonyesha ari kubwa ya wanachama kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano mpaka juhudi hizo kuonekana.

"Wanachama wamekuwa mstari wa mbele katika masuala yenye mrengo wa kijinsia, mfano tunaona jinsi wanachama wetu walivyojitoa Arusha kushiriki na kutoa elimu katika wiki ya sheria, na kuhakikisha kuwa chama kinajulikana, hili ni jambo la kujivunia kwa wanachama wote," alisema Rose.

Mtanda, alitoa rai kwa wadau wa sheria wakiwamo mahakimu kuhakikisha wanatoa haki kwa wadau wa mahakamani ili wawe na imani katika kutatua kesi zinazofikishwa mahakamani.


Ukurasa 12

**MJUE JUDITH MLUGE;**
Diwani aliyefiwa mume kwenye kampeni, madhila hadi ushindi


Ukurasa 13

Kamati Kuu CCM kurudisha jina moja spika


# siasa

JUMATANO JANUARI 26, 2021

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**KONGAMANO MATAIFA MASKINI**
## Lidhihirishe uwepo wa 'Ajenda 2063 ya Afrika Tunayoitamani'

# Sarakasi kudai tume huru, katiba mpya zinapokolea

**Na Sabato Kasika**

MWAKA 2022 unapoanza unakutana na ajenda ya muda mrefu ya kutaka katiba mpya kwa madai kuwa iliyoko haiendani na mazingira ya sasa. Kutokana na hitaji hilo vipo vyama vilivyofanya makongamano kuhamasisha katiba hiyo na vingine kutangaza kususia uchaguzi hadi itakapopatikana.

Baadhi ya wanasiasa kikiwamo Chama cha ACT-Wazalendo wanaibuka na hoja mpya kuwa 2022, utakuwa mwaka wa kudai tume huru ya uchaguzi, ili isimamie kupata katiba mpya.

Wadau wanaozungumzia msimamo huo akiwamo Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, wanasema katiba mpya ni muhimu hasa ikitokana na maoni ya Watanzania, kwani itaelekeza namna ya kupata tume huru ya uchaguzi.

"Kuwapo katiba mpya ni suala la muda mrefu ambalo tumekuwa tukilisisitiza, na tunatambua kuwa ndiyo itakayotoa mwelekeo wa tume huru itakavyopatikana," anasema Mnyika.

Anaongeza kuwa mwaka jana CHADEMA ilipanga kufanya makongamano nchi nzima kudai katiba mpya, lakini imeshindikana, japo nia ya dhati kudai katiba mpya ipo kwa sababu inajua umuhimu wake, ndiyo maana iliendesha kampeni za ndani na nje kwa kutumia mitandao ya kijamii kuidai.

Katibu Mkuu huyo anasema, hitaji la CHADEMA ni nchi kuwa na katiba mpya, siyo tume huru ya uchaguzi, kwa sababu katiba ikipatikana, italeta tume huru ya uchaguzi.

**KATIBA NI MAMA**

Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas




Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Dorothy akiwa kwenye majukumu ya siasa. **PICHA: MTANDAO**

Ngawaiya, anasema taasisi kama tume huru ya uchaguzi zinaainishwa ndani ya katiba na kwamba ni muhimu kuanza na katiba kwanza.

"Kama inakuwa vigumu kuwa na katiba mpya, hata hii iliyopo inaweza kuwekewa kiraka ikazalisha tume huru ya uchaguzi, kwani katiba ndiyo sheria kuu hivyo ianze kutafutwa kwanza," anasema Ngawaiya.

Anafafanua kuwa ndiyo inaayoelekeza tume ya huru ipatikaneje, wajumbe wake na majukumu yote na kwamba inatengenezewa kanuni na taratibu zinazoanzishwa na katiba.

"Kinachotakiwa ni vyama vya siasa na wadau wengine kuishauri serikali kukubaliana na hilo na kuitisha mjadala wa kitaifa kufikia upatikanaji wa katiba hiyo," anasema na kuongeza kuwa linabakia jukumu la serikali kuridhia au kukataa kulingana vile itakavyoona.

"Serikali ikikataa mjadala, vyama vya siasa na wadau wasishinikize, waendelee kutafuta njia sahihi za kudai kwani Watanzania wengi ninaamini wanaitaka, siyo kuhangaika na tume huru ya uchaguzi, " anasema.

**MABADILIKO HAYAKWEPEKI**

Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bobu Wangwe, anasema mabadiliko yoyote yale yawe ya kifungu kimoja cha sheria yana umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi.

Anasema, katiba mpya ni muhimu ili kuleta mabadiliko ya kimfumo, na kwamba yeyote anayetaka mabadiliko kama ACT-Wazalendo wanavyokazania kuwapo tume huru, ni jambo jema.

"Sitaki kuamini kwamba wameitelekeza ajenda ya katiba, bali ni mkakati wao wa kupambana ili kupata katiba mpya, hivyo wanachofanya ni sehemu ya mapambano hayo," anasema Wangwe.

Hata akiwapo yeyote anayekwenda mahakamani kupinga vifungu vya sheria, atamuunga mkono, kwa madai kwamba hatua hiyo inalenga kufikia mabadiliko ya demokrasia, anasema.

"Kwa hiyo ninaunga mkono juhudi za ACT-Wazalendo, kwani ninaamini hawajaitupa ajenda ya katiba mpya, ingawa wadau wote wangeelekeza nguvu zao kudai katiba kwanza," anasisitiza.

**2022 NI TUME HURU**

Chama cha ACT-Wazalendo kinasema mwaka unaanza kwa na hoja ya kutaka tume huru ya uchaguzi ili kuweka mazingira ya kupata katiba mpya inayotokana na matakwa ya Watanzania.

Kaimu Mwenyekiti wake, Dorothy Semu, anasema msimamo wao upo bayana, na kwamba sababu za kuhitaji tume hiyo ziko wazi. "Tunataka mchakato wa kura ya maoni ya Katiba mpya usimamiwe na tume huru na pia kwa kuzingatia ukweli kuwa kupatikana kwa katiba mpya na kuanza kutumika kunahitaji muda zaidi."

Semu anasema, chama hicho kinataka uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na mkuu wa 2025 usimamiwe na tume huru ya uchaguzi, huku akitaja utaratibu wa kupatikana kwa tume hiyo.

"ACT- Wazalendo inapendekeza sheria mpya ya uchaguzi 2022, iweke utaratibu kuwa, Watanzania wanaotaka kuwa wajumbe wa tume huru ya uchaguzi waombe kazi kwa tangazo la wazi kwa umma," anasema.

Semu anasema, sheria hiyo ianzishe kamati maalum ya uteuzi wa mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wa tume huru ya uchaguzi, na kwamba uteuzi ifanye usaili, iwe na uwazi kwa waombaji wote na kuchuja majina ambayo yatapelekwa kwa rais kwa ajili ya uteuzi.

"Baada ya wajumbe wa tume huru ya uchaguzi kupatikana wataajiri mkurugenzi wa uchaguzi ambaye nafasi itatangazwa, kufanyiwa usaili wa wazi na jina kupelekwa kwa Rais kuteua mkurugenzi wa uchaguzi," anasema.

MJUE JUDITH MLUGE;

# Diwani aliyefiwa mume kwenye kampeni, madhila hadi ushindi

• Akumbuka kupingwa, kisa jinsia yake • Leo! Adai mwaka kazini kaibua mengi • Kitaifa, yumo diwani 6 bora kinamama

**Na Julieth Mireri,** KIBAHA

"HAKUNA kipindi kigumu nilipitia katika harakati zangu za kisiasa kama Septemba mwaka 2020, nilipofiwa na mume wangu nikiwa kwenye kampeni za kuomba kuchaguliwa niwe diwani wa Mbwawa. Yalisemwa mengi hata kuambiwa nimemuua mume wangu.

"Nilipokea kila aina ya matusi hakuna faraja niliyoipata zaidi ya maneno ya kuumiza, kila mmoja alisema lake huku akitambua napitia wakati mgumu ambao umekuja katika kipindi changu nikiwa napambania kupata nafasi ya Diwani wa Kata ya Mbwawa kwa mara ya kwanza," anatamka mwanamama Judith Mluge.

Leo hii amefuzu kuingia katika orodha ya madiwani 14 wa kata ndani ya Halmashauri ya Mji Kibaha, pia ni sehemu ya madiwani wanawake 10 mkoani Pwani, waliopenya kuptia kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Kabla ya kugombea nafasi hiyo alikuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Halmashauri ya Mji wa Kibaha, nafasi aliyoipata mwaka 2017.

Judith anasema aliamua kuachia nafasi ya uenyekiti wa UWT baada ya kupata maoni kutoka kwa wananchi wengi wa Mbwawa wakimwomba kugombea nafasi ya diwani baada ya kushuhudia kazi mbalimbali alizokuwa akiwafanyia.

Anaeleza baada ya kuwashinda wagombea tisa aliochuana nao katika kura za maoni wapo waliokata rufani dhidi yake ndani ya chama, lakini akabaki hata kufikia hatua ya uchaguzi akipeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi mkuu wa mwaka juzi.

Mama huyo anasimulia mtihani aliyokutana nayo ndani ya chama, wapo waliomkataa kumuunga mkono na wakaungana na mpinzani kutoka chama kingine.

"Niliumia kwa niliyokuwa nayapitia, wengi walikuwa wananipinga kwa kuwa mwanamke. Hawakutaka kuniunga mkono kabisa..." anasimulia Diwani Julieth.

Anaendelea: "Walinisema vibaya, lakini sikukata tamaa kwa kuwa tayari niliamua kusimama nibadilishe mawazo ya kumdharau mwanamke katika kata yangu, niwaonyeshe naweza kufanya kazi kuliko hata mwanaume."

### MKASA ULIPOMFIKA

Diwani huyo anasimulia wakati anapambana na vikwazo hivyo akishirikiana na viongozi wa CCM kata na wilaya, akapatwa na madhila magumu ya kufiwa na mume aliyekuwa anaumwa kwa muda mrefu.

"Nilisitisha kampeni zangu na kukaa nyumbani kwa maombolezo. Lakini, mbali ya maumivu ya kuondokewa na mume, maneno ya watu yalikuwa yananiumiza sana," anatamka Julieth, akitaja mfano kashfa kuhusu kifo hicho kulichompa hisia kutaka kujiengua.



Diwani wa Mbwawa, Judith Mluge, akiwa na baadhi ya wazee muda mfupi baada ya kikoa cha Baraza la Madiwani. **PICHA ZOTE: JULIETH MKIRERI**

> "Walinisema vibaya, lakini sikukata tamaa kwa kuwa tayari niliamua kusimama nibadilishe mawazo ya kumdharau mwanamke katika kata yangu, niwaonyeshe naweza kufanya kazi kuliko hata mwanaume.



Diwani Judith Mluge, akiwaonyesha wananchi kitabu kinachoelimisha vipaumbele atakavyoshughulikia ndani ya miaka mitano ya uongozi.

Hata hivyo, anasema baada ya maombolezo, alirejea kwenye kampeni hata akachaguliwa udiwani kuwakilisha kata ya Mbwawa.

### BAADA YA KUCHAGULIWA

Anaeleza wakati anaomba nafasi hiyo kuna mambo aliyoyalenga kusimamia, ikiwamo ujenzi wa kituo cha afya katika kata yake, kwani wananchi wanatumia zahanati isiyokidhi mahitaji yao.

Pia anavitaja vipaumbele vya kampeni zake vinajumuisha ukuzaji sekta za elimu, maji na umeme, pia ujenzi wa daraja kuvuka Mto Ruvu, ambalo limekuwa likiwapotezea maisha baadhi ya wakazi wanapovuka kwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Judith anasema, pia amedhamiria kupambana na tatizo analoliita 'uongozi wa mazoea' kwenye kata hiyo, akitaka mabadiliko ya ufanyaji kazi kwa bidii kuondolea umma kero.

### MATUNDA YA MWAKA

Anataja mavuno ya bidii yake ni kujengwa ofisi ya serikali ya kata, kazi iliyokwama katika kipindi cha miaka mitatu sasa baada ya msamaria kutoa eneo, hata viongozi kufanya vikao chini ya miti na wakati mwingine kwenye vyumba vya kupanga.

Pia diwani anasema ameshafanikisha upatikanaji eneo la ujenzi wa kituo cha afya, pia ameshafanikisha maombi ya ujenzi wa daraja kwa Wakala wa Taifa wa Barabara (TANROADS) mkoa wa Pwani, huku akitaja pia kufanikisha kupatikana kwa ajili ya kujengwa kituo cha polisi katika kata yao.

Judith anajivuna anaingia katika orodha ya madiwani sita wanawake waliotambuliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao), kutokana na kazi zake kuonekana.

TGNP Mtandao ina utaratibu wa kuwatambua kinamama viongozi kuanzia ngazi ya kata wanaonufaika na mafunzo ya uongozi na kujengewa uwezo, kisha wanabadilishana uzoefu, mwaka madiwani sita ndio wametambuliwa kitaifa.

### WANUFAIKA JE?

Zena Pembe, anayeishi Miswe katika kata ya Mbwawa, Kibaha, anamwelezea Judith alimtathimini katika umahiri wa kipekee.

"Ni mwanamke tofauti, msikivu na asiyebagua watu wa kufanya nao kazi, tutaendelea kushirikiana naye kuleta maendeleo," anasema.

Pia Juma Ramadhani, anayeishi Miswe, anamtaja diwani huyo ni kati ya wanawake wasiokata tamaa wanapokutana na vikwazo dhidi ya mipango yao ya maendeleo.

"Aliwahi kugombea nafasi ya Diwani Viti Maalumu alipokosa hakukata tamaa, aliendelea na kazi za kujitoa kushirikiana na wananchi.

Mkazi mwingine, Jordan Ngairo, anamwelezea Judith ana upekee wa kutoweka madraja ya mtawala na mtawaliwa, akiwashirikisha wananchi kwa kila jambo, akiwa na tabia ya kupata ushauri kabla ya utekelezaji husika.

"Huyu diwani kwa kipindi chake hiki kifupi amefanikisha kukomesha utoro kwa wanafunzi na walimu na kumfanya kila mmoja kusimamia nafasi yake kama inavyotakiwa.

"Amekuwa akikutana na walimu mara kwa mara, pamoja na wanafunzi kuzungumza nao kusikiliza kero zao na kujadiliana kwa pamoja namna ya kuzitatua hii haijawahi tokea," anasema.

Mwingine Gabriel Kiula anaunga mkono kwa tafsiri kwamba "TGNP Mtandao haijakosea kumtambua Judith kutokana na kazi anazofanya kwa jamii."

Hapo anarejea muda mfupi wa uongozi wake kwenye kata hiyo, ameshaanza kuleta matumaini ya mapambano kutatua kero za wananchi.

"Tangu Halmashauri ya Mji wa Kibaha iundwe, hajawahi kutokea diwani mwanamke kwenye kata. Judith ni wa kwanza, pia ni mfano wa kuigwa na madiwani wengine kwa namna anavyofanya kazi zake," anaeleza Kiula.

Agustino Mdachi ni Diwani wa Kata ya Pangani, anayemwelezea Judith kuwa ana tabia ya kuguswa kwa ukaribu na matatizo ya wananchi, kisha anapambana kuyatatua, akishirikisha ushauri wa madiwani wenzake.

# Kamati Kuu kurudisha jina moja spika, kabla watiania kujinadi

## • Yadhihirisha ukaribu Samia, Magufuli

Na Ani Jozeni

BAADHI ya maswali ambayo yanaendelea kuulizwa kwa hisia tofauti na baadhi ya wachambuzi au zaidi wanaharakati, yalijibiwa wiki iliyopita wakati Kamati Kuu ya CCM ilipoketi kujadili waliochukua fomu na kujaza kuwania nafasi ya spika wa bunge.

Ni kuhusu kiasi ambacho taratibu za kawaida za mfumo wa kidemokrasia ndani na nje ya bunge zingefuatwa. Kimsingi hapakuwa na wasiwasi kuwa utaratibu wa kawaida za kuchukua fomu, kuchujwa halafu walioopita wajieleze kwa wabunge ungefuatwa kama ulivyo, lakini haikuwa hivyo.

Kilichotokea ni kudhihirisha kuwa bado hisia za nini kinachofaa zilizoinuliwa wakati wa awamu ya tano zinaendelea. Hivyo kuna kitu kama 'kazi iendelee' katika usimamizi wa shughuli za siasa nchini, kuwa demokrasia ifuatwe kwa kiwango kinachohitajika kikatiba.

Pale ambapo kuna suala la kufanyia maamuzi katika kikao, lisifumuliwe tu ili kukidhi mifumo ya demokrasia, kuruhusu wagombea au watia nia na wapambe wao waendeleze makundi.

Mfumo huo ulikuwa umezoeleka kwa wanasiasa ndani na nje ya CCM na bunge, na siyo mzaha kusema kuwa takriban kote ulikotumika ulileta udhaifu wa dhamira na uharibifu kiitikadi katika kutimiza matakwa yake.

Tatizo ni kuwa mfumo wa uchaguzi wa wazi na ushindani kati ya wanaotaka nafasi hizo unakubalika kwa sababu ya demokrasia, yaani uhuru wa watu kuchagua mgombea wanayemtaka. Ila wanaotaka kupata nafasi hiyo wana maslahi binafsi yanayooana na ya makundi kadhaa, na kundi moja likishindwa siyo rahisi kufuta majeraha kama ushindani ulikuwa mkubwa.

Kamati Kuu kwanza iliruhusu kuchukua fomu, halafu ikatupilia mbali mpangilio mzima wa kujieleza ili chama kisijitwishe zigo jipya la mivutano inayotokana na kujiuzulu kwa Spika Job Ndugai na halafu kuchaguliwa mwingine nafasi hiyo.

Ingekuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, anataka kufuata mwelekeo wa kidemokrasia angeruhusu wagombea wachujwe halafu wapate nafasi ya kujinadi mbele ya wabunge.

Kila mmoja angeelezea uzoefu wake na hata hisia zake kuhusu uendeshaji wa mhimili huo wa dola. Ni mwelekeo ambao pengine unalea udhaifu mwingine wa kuchagua spika ambaye ajenda yake ya jinsi ya kuendesha bunge imekubaliwa na wabunge.

Hali halisi ni kuwa wabunge wa chama fulani wanakuwa chini ya maekelezo ya chama hicho, na siyo bunge lijitungie kanuni za kujiendesha.

Kutoa nafasi kwa wagombea tofauti wa nafasi hiyo kutoka CCM kujieleza ni kurudisha rasmi makundi ndani ya bunge, udhaifu ulioanzia katika mchakato wa kumpata mgombea wa CCM katika uchaguzi mkuu mwaka 2005.



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MAKTABA**

Licha ya kuwa mwaka 1995 waliotaka kuteuliwa kushika bendera ya CCM walichukua fomu na kuchujwa, ilikuwa mapema kwao kuunda makundi. Mfumo wa vyama vingi ulirudishwa mwaka 1992 kukawa na miaka miwili tu ya maandalizi, na wakati wanafikia miaka mitatu ya kupiga kura, si maandalizi tena. Wakajipanga vyema miaka 10 iliyofuata na hata 1995 walikuwa na ubavu kiasi fulani lakini Rais mstaafu, Mwalimu Julius Nyerere akawa mwenyekiti wa jopo, akawatoa.

Mwaka 2005 wakiwa wamejiandaa kikamilifu na kundi moja liliposhinda likawa linawindana na lililoshindwa au yaliyoshindwa, kwa vita ya mapana na marefu tofauti. Halafu kundi la aliyepewa bendera ya CCM likaingia katika vita ya ndani kwa ndani nani atakayechukua kijiti mwaka 2015 wakati aliyeshinda akiacha kiti wazi baada ya mihula miwili.

Vita ikaelekezwa kwa kundi la wasindikizaji lililosaidia kupata ushindi ndani ya CCM, hivyo kukawa na vita ngazi za juu. Aliyeko madarakani akichochea harakati dhidi ya msaidizi wa karibu na swahiba wake mkuu ambaye kiasi fulani alikuwa mwezeshaji wa kundi hilo kwa jumla, wakati wa harakati za kupata ushindi CCM na miongoni mwa wapigakura.

Upinzani ulitumika kuzua masuala ambayo serikalini yanaeleweka yalifanywa kwa sababu zipi, tena zinazoendana na sera za uchumi au mikakati ya kiusalama.

Ila yanaletwa kwa wananchi kama hujuma tena kwa mshangao mkubwa, ionekane kuwa rushwa imekithiri, si ya serikali nzima ila watu kadhaa tu.

Dhoruba hii ilipofikia uchaguzi mkuu unaofuata ambako kiti cha rais kiko wazi ikafikisha hali ya chama kutaharuki, yalipokatwa majina yote muhimu wakabaki 'wadandiaji' wenye sifa kiasi katika chama, na uzoefu serikalini uliokuwa unapishana, wengine waobezi na baadhi 'wakuja' tu.

CCM ikawa hatarini kumeguka baadhi ya makada wakimfuata mgombea aliyekatwa na kuhamia upinzani baada ya kutolewa madarakani awali. Aliyeshinda uchaguzi aliangalia yote hayo akajua tatizo la kupigana vikumbo kutafuta rafiki yenu atakayewaweka katika nafasi nyeti kutumika kwa maslahi binafsi zaidi.

Ndipo alipoingia madarakani akaanza 'kutumbua majipu,' kuvuta mazulia waliokalia wakubwa ambao nafasi zao zinawezesha wadau tofauti mambo yao yaende vyema kutokana na kupindisha sheria au kuweka kanuni mbovu sekta tofauti.

> Upinzani ulitumika kuzua masuala ambayo serikalini yanaeleweka yalifanywa kwa sababu zipi, tena zinazoendana na sera za uchumi au mikakati ya kiusalama.

Kampeni hiyo ililazimisha kupigwa 'stop' kwa mtiririko wa kawaida wa siasa za vyama vingi, ili kulinda mwelekeo mpya wa dola usisumbuliwe na kubughudhiwa dola likisimamia maelekezo ya uchaguzi umekwisha sasa tufanye kazi.

Uchambuzi dhaifu kwa miaka kadhaa umebaini kuwa ni maamuzi ya kiongozi aliyekuwpo kutokama na hulka yake ya ukali, au tamaa ya udikteta.

Kumbe ukitaka serikali ibaki katika maadili na siasa ilenge maendeleo na si kujuana katika kuchaguana ili baadaye mambo yawe safi kwa kila mhusika, lazima ubane mpangilio wa kidemokrasia ikibidi uwe butu.

Tayari tanzia kadhaa zimeshaandikwa kuhusu uendeshaji wa shughuli za bunge kama mhimili wa kuisimamia serikali, huku suala la wabunge 19 wa viti maalum waliopoteza uanachama wao CHADEMA, likitajwa sana kama mojawapo ya masuala yanayomngoja spika ajaye.

Sasa inaelekea suala hilo litapigwa kalenda kwani hoja za spika mstaafu zitakuwa bado zina nguvu za kisiasa, pale dhamira ya utawala bungeni ikiwa haijabadilika.

JUKWAA LA VIONGOZI

KONGAMANO MATAIFA MASKINI

# Lidhihirishe uwepo wa 'Ajenda 2063 ya Afrika Tunayoitamani'

**Na Gaudensia Mngumi**

AFRIKA ni bara lenye rasilimali zote zinazohitajika duniani kwa ajili ya maendeleo ya sekta zote, ni eneo linaloweza kutoa nafasi kubwa na endelevu za uwekezaji kwa ajili ya maendeleo ya viwanda ya kuzalisha vifaa, bidhaa na rasilimali za kila aina. Ina miti na mimea inayofaa kwa viwanda vya dawa na pia ni baba wa ardhi inayofaa kwa kilimo hivyo kuwa chanzo cha chakula na mahitaji mengine ya lishe duniani.

Mchanganyiko wa utajiri wa kila aina kuanzia madini kama shaba, chuma, cobalt inayohitajika kwenye vifaa vya kielektroniki katika bara hilo na rasilimali ardhi inayofaa kwa kilimo ambayo haijatumiwa ipasavyo na idadi kubwa ya watu hasa vijana ambao ni nguvu kazi muhimu vinaipa Afrika uwanja wa kipekee.

Aidha, ina turufu ya kisiasa ikiwa na mataifa 54 inaweza kujisimamia kama 'bloc' au kanda kama ulivyo Umoja wa Ulaya (EU) ikiwa na ushawishi wa kura yake 54 ndani ya Umoja wa Mataifa (UN), hakuna cha kuizidi Afrika.

Ni 'bloc' au kanda inayotazamwa na mataifa kama China, Marekani, Urusi, Japan na hata Israel, ndiyo maana kumekuwa na makongamano ya mara kwa mara kati ya China na Afrika, Japan, Urusi na hata Israel yakiikumbatia Afrika.

Licha ya utajiri na kuwa kipenzi cha mataifa makubwa bado ni maskini kupindukia. Watu wake wamekuwa wahamaji wakikimbilia Ulaya na Marekani na kufa ndani ya bahari ya Mediterranean wanakoliwa na papa kila mara.

Baadhi ya nchi maskini ni mataifa yote yaliyoko Kusini ya Jangwa la Sahara kama Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi, Msumbiji na nchi za Asia kama Afghanistan, Bangladesh, Jamhuri ya Lao, Myanmar, Cambodia, Nepal na Bhutan.




Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres akiwa na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki Mahamat. **PICHA: MTANDAO**

### FURSA YA DOHA

Mwaka huu nchini Qatar, utafanyika mkutano wa mataifa maskini unaoandaliwa na Umoja wa Mataifa kushughulikia nchi maskini za Afrika zikiwa nyingi zaidi.

Doha ni fursa kwa Afrika kwa vile linatarajiwa kuwa jukwaa la namna bora ya kuzisaidia nchi maskini ili ziendelee au zihitimu (graduate) kutoka uchumi duni na kuingia kwenye uchumi wa viwanda.

Licha ya mataifa yaliyoendelea kufahamu kuwa uchumi wa dunia unaweza kunufaika na kuimarika zaidi kutokana na uwepo wa Afrika hazijaonyesha nia ya dhati ya kuisaidia kujikwamua. Lakini bara hilo halijatimiza wajibu wake, kwani linahitaji kufanya juhudi za dhati za kujiinua na kujinasua na ufukara.

> Barabara zikijengeka inamaanisha uchumi unafunguka na ndiyo mwanzo wa ajenda 2063 kufanikiwa.

Mkutano wa Doha utakaofanyika wakati wowote mwaka huu, ulitakuwa na mingine minne wa kwanza ukifanyika Septemba 1981 Ufaransa, 1990 Ufaransa, wa tatu ulifanyika Mei 2001 nchini Ubelgiji na wa nne ulikuwa Mei 2011 jijini Istanbul Uturuki.

Mchumi na mtafiti kutoka Taasisi ya ESRF ya Dar es Salaam, Dk. Hoseana Lunogelo, akizungumzia mikutano wa Umoja wa Mataifa (UN) kujadili maendeleo ya nchi maskini, akiangazia zaidi Afrika anasema, tangu miaka ya 1970 UN imeanza kuzitambua na kuzisaidia nchi maskini katika majukwaa hayo maalumu.

Anasema mkutano wa Instanbul, ulijadili utekelezaji wa makubaliano yaliyowekwa na mikutano ya awali na kuandaa mingine iliyokuwa ifanyiwe kazi kuanzia 2011.

Akirejea Afrika anasema eneo lililokuwa limepewa kipaumbele ni mataifa yaliyoendelea kuisaidia kupata nishati, kuboresha miundombinu kwa kuiunganisha miji mikuu ya mataifa hayo kupitia treni za mwendokasi.

Dokta Lunogelo, anasema licha ya kukubaliana hayo mataifa tajiri duniani kuisaidia nchi maskini kwa kutoa asilimia moja ya pato lao la taifa (GDP), mengi hayakutimizi ahadi zao.

"Lengo lilikuwa kuweka miundombinu imara, kuinua kilimo na uhakika wa chakula, kupata nishati na kujenga viwanda. Hata hivyo, fedha hazikutolewa kama zilivyoahidiwa. Japan na mataifa ya Scandinavia ndiyo yaliyochangia zaidi lakini mengine hayakutimiza ahadi hiyo."

Akizungumzia mradi wa umeme, anasema ulikuwa ujengwe kwenye bwawa la Inga nchini Demokrasia ya Congo. Hata hivyo kazi hiyo haijakamilika hadi leo.

Aidha, mradi wa kuunga miji mikuu ya Afrika kwa treni za mwendo kasi nao haujafanyika hadi sasa licha ya nchi mbalimbali kufanya juhudi binafsi za kujenga reli na barabara za kisasa.

Hivyo mkutano wa Doha, utaendelea kuangalia utekelezaji wa mikakati na makubaliano ya Istanbul.

### JUHUDI ZA AFRIKA

Miaka miwili baada ya Mkutano wa Istanbul, 2013, Umoja wa Afrika (AU), ulikubaliana kuanzisha na kutekeleza mipango ya maendeleo na mwongozo wa kushughulikia changamoto zinazolikabili bara hilo, uliopewa jina la 'The Africa We Want au Agenda 2063.'

Ajenda 2063 au Afrika Tunayoitamani, ilitanguliwa na Mkataba wa Afrika wa Demokrasia na Uongozi (ACDEG).Ukitoa maono ya uongozi bora unaozingatia demokrasia, utawala wa sheria na kuheshimu katiba, uchaguzi huru na haki, kulinda rasilimali za Afrika, kujiendeleza kiteknolojia, kuondoa umaskini njaa na magonjwa.

Aidha, ACDEG iliyozaliwa kutokana na Muundo wa Utawala na Uongozi wa Kidemokrasia Afrika (The African Governance Architecture - AGA) pamoja na

Ajenda ya 2063 vinalenga kuwa na mtangamano wa Afrika nzima.

Ikiwa na pasi ya kusafiria, viza, sarafu, soko na uongozi vyote vya aina moja . Lakini kuwa na bara lisilo na vurumai za kisiasa wala vita.

AU pia ilianza kutekeleza mkataba wa biashara huru baina ya nchi wanachama (AfCTA) ili kuimarisha biashara na uwekezaji

Kwa mujibu wa ripoti za BBC, Ajenda 2063 inataka kukamilisha kazi ya kuunganisha miji mkuu yote ya Afrika na vituo vya kibiashara kupitia miundombinu ya treni hizo.

Aidha, kuimarisha biashara baina ya mataifa ya Afrika ili kuboresha nafasi yake katika soko la kimataifa.

Kuzalisha kilowati 42,000 za umeme kutoka bwawa la Inga nchini DR Congo ili kupata umeme na kuondoa changamoto za nishati na kuondoa vikwazo vya usafiri kwa Waafrika, wanaotaka kufanya kazi katika mataifa ya AU.

Mengine ni kuandaa tiketi na usafiri wa anga la Afrika au the Single African Air Transport Market SAATM na kujenga chuo kikuu cha kidijitali cha Afrika.

Kuandika upya historia yake kwa kutayarisha 'encyclopedia ya Kiafrika yenye maelezo ya kuaminika na taarifa zake.

### KUANZA UTEKELEZAJI

Utekelezaji wa miradi ya Ajenda 2063 haujaanza kuonekana, lakini Afrika ina fursa ya kuitumia mikutano na mataifa kama China, Russia, Israel, Japan kupenyeza ajenda zake hizo, hususan kujenga miundombinu ya kuunganisha miji mikuu.

Barabara zikijengeka inamaanisha uchumi unafunguka na ndiyo mwanzo wa ajenda 2063 kufanikiwa.

Afrika itumie mkutano wa Doha kutekeleza mipango ya Ajenda 2063 ikitaja mbinu zake na kuweka ridhaa ya kisiasa na kuwekeza ili ifikapo 2030 ihitimu kuwa Afrika ya viwanda na si bara la ufukara.

Lakini suala la migogoro kama vurumai za Sudan, Burkina Faso na Ethiopia zitamalizwa kwa wanachama wa AU kusaini mkataba wa ACDEG na kuwa na Afrika yenye demokrasia.





# Waziri Chana: Changamkieni kwenye Agosti

**Na Peter Mkwavila**, DODOMA

WANANCHI wamehimizwa kujitokeza wa wingi kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti mwaka huu, ili kupata takwimu sahihi kwa maendeleo ya taifa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Pindi Chana, alipofanya kikao na Ofisi ya Taifa ya Mtakwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kuhusu maandalizi ya sensa ya watu na makazi.

Waziri Pindi alisema kuna umuhimu mkubwa wa kufanya sensa hiyo kwani itatoa takwimu muhimu ambazo serikali itazitumia kufahamu mahitaji ya wananchi wake na miundombinu inayotakiwa kuboreshwa ili wananchi kupata huduma muhimu.

"Takwimu hizi tunaweza kuzitumia kwa maendeleo yetu wenyewe, kuna masuala ya ujenzi wa vituo vya afya, madarasa, uwekezaji wa aina mabalimbali na hata uchumi wa mtu mmoja mmoja unahitaji kujua idadi ya watu na makazi wakati umefika sasa tuendele kuhamasishana na kuelekezana kufafanua masuala haya ya sensa," alisema Chana.

Pia aliagiza kamati za sensa za mikoa, wilaya, kata na vitongoji kuundwa na kukutana kujadili masuala mbalimbali kuhusu maandalizi ya utekelezaji ya sensa hiyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa manufaa ya wananchi.

"Kamati hizi ziwe zimeshaundwa na kukutana kuandaa maandalizi ya utekelezaji wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 nalo ni jambo la msingi na wajumbe wa kamati za sensa nao wakutane waanze kutafakari masuala ya maandalizi na namna shughuli itakavyofanyika," alieleza.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa maandalizi ya serikali ya kuwezesha bajeti ya masuala ya sensa, huku akiishukuru Serikali ya Zanzibar kwa ushrikiano mkubwa inayoonyesha kuhakikisha sensa inafanyika kwa ustawi wa nchi.

Naye Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi Zanzibar, Balozi Mohamed Haji Hamza, alibainisha kuwa sensa hiyo itashirikisha makundi yote wakiwamo vijana, watu mashuhuri, nyumba za ibada na viongozi wa kisiasa kufikisha ujumbe uliokusudiwa na kuhakikisha kila mwananchi anashiriki sensa.

"Tutaendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika sensa tutatumia makundi yote makanisani, misikitini, wapo wasanii, wastaafu na kila yakapofanyika maadhimisho ya kitaifa nia yetu wananchi wapate taarifa ya sensa na umuhimu wake na mashirika ya umma pamoja na maeneo yote yenye mkusanyiko wa watu na vyombo vya usafiri," alifafanua Balozi Hamza.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alieleza kwamba sensa ya mwaka huu itafanyika kidigitali kupata taarifa sahihi na kwa wakati kulingan ana madodoso yanavyoelekeza ambapo tayari sensa ya majaribio imefanyika na elimu kuhusu sensa imetolewa kwa makarani wa sensa kuwajengea uwezo wa kukusanya taarifa kama inavyotakiwa.

"Makarani watakaokusanya taarifa hizi za makazi, majengo na watu tunawapa elimu namna ya kuuliza maswali kulingana na hali ya mtu aliyonayo hasa wenye ulemavu na sensa ya majaribo tuliyofanya imetupa mwaka mkubwa wa kile tunachoenda kukifanya na sensa hii itagusa hadi ngazi za vitongoji," alisema Dk. Albina.

# Wanawake TAWOMA wahamasishwa kushiriki katika uchimbaji madini

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amewataka wanawake kujitokeza kwa wingi kushiriki katika shughuli za uchimbaji madini badala ya kuendelea kubaki nyuma katika sekta hiyo inayochangia kiasi kikubwa katika pato la taifa.

Biteko, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa 24 wa Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini Tanzania (TAWOMA). Alisema wanawake nchini wanapaswa kuwa vinara katika kushiriki shughuli za uchimbaji wa madini na kuacha kuendelea kuona kuwa kazi hiyo ni kwa ajili ya wanaume pekee.

"Mnapaswa kuwa kinara kwenye madini acheni kujiona duni kwani sekta ya madini si kwa ajili ya wanaume tu... shughuli za uchimbaji hata nyie mnaweza kuzifanya tena kwa ufanisi mkubwa," alisema Biteko.

Kadhalika, alisema wanawake hawapaswi kuwa sehemu ya watazamaji katika sekta hiyo, bali kuwa mstari wa mbele katika kushiriki shughuli za uchimbaji na kutoa mchango katika ukuzaji wa pato la taifa kupitia sekta hiyo.

"Tuondoe dhana ya kwamba shughuli za uchimbaji wa madini ni za wanaume na anayepaswa kupewa leseni za uchimbaji ni mwanaume, hapana wanawake wakiingia katika sekta hii sehemu kubwa ya jamii itanufaika na sekta hii ya madini," alisema Biteko.

Aidha, alizitaka taasisi za kifedha kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo wanawake kwa kuwa ni waaminifu katika masuala ya fedha kuliko wanaume.

"Simaanishi kuwa wanaume si waaminifu, lakini wanawake kuna kitu Mungu amewapa ambacho sisi wanaume hatuna, hata takwimu za watu ambao wanaotorosha madini idadi kubwa ni wanaume, wanawake ni wawili tuu hadi sasa," alisisitiza Biteko.

Waziri Biteko alisema serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wanawake wachimbaji wa madini ili kuzifikia ndoto zao.

"Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeweka mkazo katika sekta hii hivi sasa hata katika usafirishaji wa madini Watanzania wanahusika, zamani ilikuwa ukitaka uchimbe madini hadi mtu fulani aseme," alisema.

Katibu Mkuu wa TAWOMA, Salma Kundi, alisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa wataalamu wa masuala ya madini.

"Changamoto nyingine mgeni rasmi ni ukosefu wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya uchimbaji madini, teknolojia ya uchenjuaji, ukosefu wa umeme katika maeneo ya uchimbaji na kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara katika maeneo ya uchimbaji madini," alisema.




Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Kuu ya Tanzania, Mustapha Siyani (katikati), akikata utepe kuzindua Mahakama ya Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# TPA: Wananchi wajifunze fursa za bandari

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imehimiza wananchi kujifunza kuwapo kwa bandari na fursa zake ili kuchochea uchumi kupaa.

Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria TPA, Stanslaus Kagis, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza uwapo wao katika Wiki ya Sheria inayoendelea mkoani hapo.

Alisema wamefika katika maonyesho hayo kutokana na kuthamini mchango wa mahakama na sheria katika uendeshaji wa mamlaka hiyo yenye kazi ya kuendesha bandari zote nchini zikiwamo bandari bubu.

Alisema mamlaka hiyo ipo kisheria na uwapo wao katika wiki ya kisheria imelenga kuwaelimisha watu utendaji kazi wao, sheria inayofanya wafanyekazi na mchango wao kwa umma. Aidha, alisema mamlaka hiyo inakaribisha Watanzania kuona fursa zinazopatikana na uwapo wa bandari nchini katika kujikweza kiuchumi wao binafsi na taifa kwa jumla.

"Tupo kuwaelimisha Watanzania kuhusu bandari zetu, fursa zilizoko katika uchumi wa bandari na pia wajue hili ni lango la kiuchumi," alisema Kagisa. Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eric Hamissi, alisema watatumia Wiki ya Sheria kukutana na wadau mbalimbali wa biashara na sheria na kuwaonyesha fursa za wao kuchangia katika huduma za bandari.

Alisema pia banda lao lina wataalamu wengi ambao watakuwa tayari kujibu maswali yote wasioyaelewa kuhusu huduma za bandari.





# Wakulima wadogo wapewa elimu ya kilimo cha pilipili

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WAKULIMA wadogo 200 wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, wamepatiwa elimu ya kilimo cha mkataba kwa kuzalisha zao la pilipili kichaa ili kukuza uchumi na kuachana na kilimo cha mazoea cha kutegemea mvua.

Mkurugenzi uendeshaji wa kampuni inayojihusisha na kilimo mkataba kwa wakulima wilayani Rungwe ya Sales Bridge, Wende Mubepi, juzi alisema kuwa wameanza mradi huo wilayani humo baada ya kufanya utafiti wa udongo na kubaini kufaa kwa kilimo cha pilipili.

"Awali kilimo hiki kilitumiwa sana na wakulima wakubwa kutokana na kuwapo kwa fursa kubwa kiuchumi kwa kulitambua hilo tumeamua kuwaingiza na wakulima wadogo ili nao waanze kilimo hicho kwa kushirikiana na Kampuni ya Oittese, tumewafikia wakulima na kuwasajili kwenye mifumo ya kidigitali kabla ya kuanza uzalishaji itakayotuweza kupata takwimu halisi ya wazalishaji," alisema Mubepi.

Aliongeza wameweka utaratibu mzuri wa kimifumo kwa kuwakopesha mbegu na wanawekeana dhamana wenyewe na wakati wa kuingizwa sokoni ndipo wanakatwa mkopo wa mbegu.

Mkulima Lamson Zebedayo, alisema kuwa kilimo hicho kimekuja wakati mzuri kwa wakulima kutokana na kuwapo kwa masoko ya uhakika hivyo kusisitiza kampuni zinazosambaza mbegu kutoa elimu zaidi ya uoteshaji vitalu kitaalamu ili waweze kuzalisha kwa wingi.

Ipyana Mwagundama, mkazi wa Nditu, alisema kuwa ni wakati sasa wakulima kujikomboa kiuchumi kufuatia zao la pilipili kichaa kutokana na kuwapo kwa soko la uhakika kupitia kampuni hiyo inayoingia kilimo mkataba na wakulima.

Alisema kuwa kupitia fursa hiyo wakulima wapatiwe elimu ya namna ya kuandaa mashamba, kuzalisha vitali na mpaka wakati wa mavuno jambo ambalo litaleta msukumo mkubwa wa kuendeleza kilimo hicho mkataba kwa wakulima.



Mtendaji wa Kata ya Ngonga, wilayani Kyela, mkoani Mbeya, Lutufyo Mwangamilo (katikati), akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha afya, unaotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya hiyo, kwa fedha za mapato ya ndani, wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, hivi karibuni. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wachimbaji wadogo watakiwa kujiunga kwenye vikundi

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

MBUNGE wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, amehamasisha wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu kujiunga kwenye vikundi ili waweze kupata mikopo ya asilimia 10 na kuanzisha miradi mingine ya kiuchumi.

Akizungumza na Nipashe jana wakati wa mahojiano kuhusiana na utaratibu wa kuwezesha vijana hususani wachimbaji wadogo kufuatia kilio chao cha kuomba mikopo, ili kubuni miradi mingine licha ya shughuli za uchimbaji ambazo zina athari kubwa kiafya.

"Nawaomba wananchi hususani vijana ambao shughuli zao za uchimbaji wa madini, vibarua na biashara zingine wajiunge kwenye vikundi fedha zipo kwenye halmashauri na ni sera ambayo inaelekeza mikopo asilimia 10 zielekezwe huko ikiwa ni pamoja na walemavu," alisema Kasaka.

Aidha, alisema kuwa akiwa kama mwakilishi wao amejipanga kuhakikisha vijana wanakuwa na miradi ya kiuchumi mbali na kazi kwenye migodi na hata kujihusisha na uchimbaji mdogo wa madini.

"Sera inaelekeza vijana, wanawake na wenye ulemavu wapate mikopo hivyo ni wakati wao sasa kuchangamkia fursa hiyo, ili kwenda sambamba na kauli mbiu ya serikali ya hapa kazi tu," alisema.

Mchimbaji wa Mdogo wa Madini Kata ya Matundasi, Emmanuel Jackson, alisema kuwa shughuli za uchimbaji wa madini zinahitaki mtaji mkubwa hivyo wanaiomba serikali kuwapatia mikopo ya vifaa vya kisasa ili kwenda na wakati na si uchimbaji wa kubahatisha.

"Shughuli za madini hazihitaji fedha mkononi hivyo tupatiwe mikopo ya vifaa vya utafutaji uchimbaji kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuachana na kuchimba kwa mazoea," alisema Jackson.

# NIMRI yaombwa utafiti maeneo uchimbaji madini

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

TAASISI ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), imeombwa kufanya utafiti katika maeneo ya uchimbaji wa madini Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya ili kusaidia wananchi kutambua athari zitokanazo na matumizi ya vitu vyenye kemikali kwa kubadili mifumo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Daison Andrew, jana alisema kuwa uchimbaji wa madini wa sasa una athari kubwa kwa jamii hivyo kuna kila sababu kufanyika utafiti kwa kuzingatia sera ili jamii ipatiwe elimu na madhara ya matumizi ya vitu vyenye kemikali hususan maji wanayotumia kuchenjua dhahabu.

"Jamii ikipatiwa elimu na kukubali kubadili mifumo ya uendeshaji wa maisha pia itasaidia maeneo hayo kubadili matumizi ya uwekezaji mwingine na kuokoa maisha ya wananchi wa chunya kuna kitu cha kufanya kwa siku za mbeleni kwa watu kubadili mifumo ya maisha kwa kuachana na shughuli ambazo kwa namna moja ama nyingine zinahatarisha usalama wao kwa kuwa katika hatari ya kuibua magonjwa ya kansa na kifua kikuu,"alisema Andrew.

Alisema katika maeneo hayo pia kuna ugonjwa wa kifua kikuu na kwamba yote hayo yanastahili kufanyiwa utafiti na itasaidia kukoa maisha ya wananchi wa Chunya.

Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, alisema kuwa kila jambo linastahili ushirikishwaji na hivyo watashirikiana ili kuona namna ya kuwafikia kufanya utafiti kwa kina kuhusiana na tatizo hilo.

Mkazi wa Itumbi, Elika Salomon, alisema kuwa suala la magonjwa katika maeneo yanayojihusisha na shughuli za uchimbaji madini ni kubwa kwani changamoto kubwa ni matumizi ya maji wanayotumia si salama.

"Kwa mfano huku porini Itumbi hakuna huduma ya maji, hivyo tunayatafuta kwenye mifereji au mito, msimu huu wa mvua walau tunashukuru tunakunywa maji yaliyo masafi, hivyo tunaomba serikali kuona namna ya kutusogezea huduma ili kunusuru maisha yetu," alisema.



## Hukumu kesi nyumba zilizotaifishwa Mapinduzi Jan. 27

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KESI ya madai ya kurejeshwa nyumba iliyotaifishwa na serikali baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 katika Mtaa wa Mladenge, iliyofunguliwa na Sultanali Abdalla Gulam Hussen dhidi ya wadaiwa watano, inatarajiwa kutolewa hukumu na Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Bwana Isaya Kayange, Januari 27.

Awali hukumu hiyo ilikuwa itolewe Januari 20, lakini ilikwama kutokana na kutokamilika kuandikwa na Hakimu Kayange.

"Hukumu ya kesi ambayo nilikuwa nitoe leo badala yake itasomwa Januari 27, lakini sio katika jengo la mahakama hii itakuwa katika jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu," alisema Hakimu Kayange.

Katika kesi hiyo mlalamikaji Sultanali, amelazimika kukata rufani kupinga uamuzi uliotolewa na Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Aziza Iddi Suweid, katika mapitio ya hukumu ya awali iliyokuwa imetolewa na aliyekuwa Jaji wa Mahakama Kuu, Abraham Mwampashi, ambaye sasa ni Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania.

Jaji Mwapashi katika hukumu yake alimpatia ushindi na kuwataka wadaiwa kuhakikisha wanahama katika nyumba namba 3043 na 3044, lakini mdaiwa Razaki Mahamoud Hussen, alikata rufani akipinga nyumba namba 3041 kuhusishwa katika hukumu wakati hakuwamo katika hati ya kiapo cha madai ya mlalamikaji.

Akitoa hukumu Oktoba 10, mwaka 2020, Jaji Aziza Iddi Suweid, alisema mahakama inaiachia nyumba Na. 3041 baada ya kujiridhisha imechukuliwa kimakosa na badala yake utekelezaji uendelee kwa nyumba Na. 3043/44 na kama ilivyoagizwa na mahakama hiyo katika kesi ya madai Na. 19 ya 2009.

Pia mahakama iliagiza kila upande katika kesi hiyo inapaswa kubeba gharama zake yenyewe.

Shauri hilo la madai Na. 24 kati ya Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) ambaye ni mdai dhidi ya Sultan Abdalla (mdaiwa) na Mahmoud Hussein Parker, Razak Mahmoud Hussein, Yussuf Ramadhan, Suleiman Yussuf na Salama Kombo (wadeni), lilifunguliwa mwaka 2020.

Kwa mujibu wa sheria ya serikali ya kutaifisha mali ya mwaka 1964, nyumba namba 3,141 ilitaifishwa na serikali wakati ikimilikiwa na Abdullah G Gowani pamoja na nyumba saba katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.

Watu wengine ambao nyumba zao zilitafishwa na serikali ni Salum Muhsin katika mtaa wa (Kwaalamsha), Habib Vusta Punja (Mwembe Mimba), Nurdin Jivanji (Kajificheni Mji Mkongwe), Visanji Changa Bazar, Ismail Jamat (Wete), Ismail Jamat (Chake chake) pamoja na Ithnasherl (wete).

Nyumba hizo zilitaifishwa na kuchapishwa rasmi katika gazeti la serikali mwaka 1970 kwa kutumia sheria hiyo kabla ya nyumba Na. 3141 ya Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati Novemba mosi, mwaka 1989 kumuuzia Razak Mahmoud Hussen kwa thamani ya Sh. 270,000.

"Nathibitisha kuwa Razak Mahmoud Hussen, ameuziwa nyumba niliyoitaja hapo juu kwa thamani ya Sh. 270,000 na amelipa fedha hizo zote kwa stakabadhi namba 109269 ya tarehe 25/10 mwaka 1980, inaeleza barua iliyoandikwa na aliyekuwa Mkuu wa Mapato katika wizara hiyo, Kei Juma.

Kwa mujibu wa waraka wa serikali "Pamoja na barua hii ninaleta waraka wake ili ukabidhiwe nyumba yako," umesisitiza waraka wa barua wa Mkuu wa Mapato Juma.

Kesi hiyo imeibua mjadala mzito Visiwani Zanzibar kutokana na watu wengi kutaifishwa nyumba zao baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 na matokeo ya kesi yanaendelea kusubiriwa kwa shauku kubwa na wananchi.

Hata hivyo, idadi kubwa ya watu waliotaifishwa nyumba zao wakiwamo wenye asili ya Asia na Waarabu, idadi kubwa iliondoka na kuamua kuishi nje ya nchi baada ya Mapinduzi hayo hasa nchini Dubai, Uingereza, Oman na wengine kuhamia Tanzania Bara.

# Ujerumani kurejesha uhusiano na Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Ujerumani imeridhia kurejesha uhusiano baina yake na Zanzibar kuendelea kutoa misaada katika sekta za kimaendeleo ikiwamo maji.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Juma Malik Akil, aliyasema hayo jana wakati akifungua majadiliano ya pamoja baina ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Shirikisho ya Ujerumani kwa lengo la kufanya mapitio ya ushirikiano huo kwa pande zote mbili.

Maeneo mengine ambayo shirikisho hilo limeonyesha nia ya kusaidia ni sekta ya afya ya upatikanaji wa bima ya afya, uchumi wa bahari, udhibiti wa hali ya mazingira hasa ya bahari, utawala bora, sekta ya nyumba na michezo.

Alisema kurudi kwa uhusiano huo kutasaidia kwa kiasi kikubwa maeneo mengi ambayo yana changamoto ikiwamo sekta ya maji kuimarika na kuondoa changamoto hizo za kiuchumi na kijamii.

"Itakumbukwa kwamba mwaka 2015 baada ya uchaguzi mkuu Serikali ya Zanzibar iliondoa moja kwa moja ushirikiano wake na kuzuia misaada yake kwa Zanzibar na baada ya kujiridhirisha kuwa imerudi katika utawala bora, imeamua kuridhia kuja kufanya shughuli kupitia misaada ya kimaendeleo," alisema.

Katibu Juma aliwahakikishia wananchi wa Zanzibar wategemee kurudi kwa uhusiano wa asili ambao ulianza kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ikiwamo ujenzi wa nyumba za Mjerumani Kiwajuni.

"Wananchi wategemee mambo makubwa, wenzetu wamekuja kwa nia ya kutusaidia hasa katika kuimarisha huduma ya maji kwa kuwa tatizo hilo limekuwa ni changamoto kubwa katika maeneo mengi ya Zanzibar," alisema.

Akiwasilisha mada ya dira ya maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 Kamishna wa Ukuzaji Uchumi Tume ya Mipango Zanzibar, Ahmed Makame Haji, alisema Zanzibar ilikuwa inatekeleza dira ya kwanza ya mwaka 2020 ambayo ilizinduliwa rasmi mwaka 2000.

Alisema dira hiyo ina malengo mbalimbali, lakini kuu ni kuifika Zanzibar katika kipato cha kati na tayari imeshaingia.

Aidha, alibainisha kwamba dira ya maendeleo ya mwaka 2050 ni kuifanya Zanzibar iendelee zaidi na kufikia nchi ya kipato cha kati katika ngazi ya juu.

Naye Mkuu wa Ushirikiano Ubalozi wa Ujerumani, Dk. Katrin Bornemann, alisema Serikali ya Ujerumani imerudi kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wote. Alisema yapo maeneo ambayo wapo tayari kusaidia na kufanya kwa pamoja katika miradi ya maendeleo wakianza na miradi ya majisafi na salama, sekta ya afya, michezo na vijana.

Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii Jinsia na Watoto, Dhamira Mohamed na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Khamis Said, walisema kufufuka kwa ushirikiano huo baina ya nchi hizo mbili kutasaidia kwa kiasi kikubwa katika kusaidia miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.




Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khadija Said, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar juzi, kuhusu kongamano la bima la Afrika ambalo kwa mara ya kwanza litafanyika kisiwani humo, leo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## 'Falsafa ya uchumi wa buluu ikitekelezwa itainua uchumi'

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Gilbert Kalima, amesema falsafa ya uchumi wa buluu ikitekelezwa kwa vitendo itawainua kiuchumi wananchi visiwani humo.

Kauli hiyo alisema jana baada ya kufungua Tawi la Gando lililoko katika Jimbo la Gando, Wilaya ya Wete Pemba.

Alisema falsafa hiyo imejaa vitu vya msingi ambavyo vikitekelezwa kwa haraka vitawatoa wananchi katika wimbi la umaskini.

Kalima, alisema mambo hayo hasa miradi ya viwanda vidogo na vikubwa na fursa ya matumizi ya teknolojia katika sekta za uvuvi, kilimo na uwekezaji ndiyo uti wa mgongo wa kukuza kwa haraka uchumi wa nchi.

Aliwataka wananchi wa Jimbo la Gando watumie vizuri fursa ya uchumi wa buluu ili kunufaika na kipato kikubwa kitakachotokana na matumizi mazuri ya uvuvi na kilimo cha kisasa.

Kalima ambaye ni Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, alisema kwamba sera hiyo ya uchumi wa buluu iliyoasisiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, imebeba fursa za kuwakomboa wananchi kiuchumi.

Aliwataka viongozi waliopewa dhamana ya uongozi bila kujali tofauti za kisiasa wachape kazi na ndiyo kipimo sahihi cha kuwavuta wapinzani kujiunga na Chama Cha Mapinduzi, kwa sababu kitakuwa kinatoa majibu sahihi ya maswali na mahitaji yao.

Naye Mbunge wa Jimbo la Gando, Salim Mussa Omar, alisema anaendelea kutekeleza vyema ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025, kwa kuwanunulia vifaa vya uvuvi ikiwamo nyavu ili wanufaike na dhana ya uchumi wa buluu.

Alisema anaendelea kutafuta ufumbuzi wa tatizo la majisafi na salama katika maeneo mbalimbali ya jimbo hilo na ametoa vifaa vya kusambazia maji vyenye thamani ya Sh. milioni 70.

Kwa upande wa Mwakilishi wa jimbo hilo, Mariam Thani, alisema kwa upande wake ameshiriki kuchangia fedha za ujenzi katika miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya jimbo hilo.

HABARI KITAIFA

# Mjomba wa mfanyabiashara anayedaiwa kuuawa asimulia

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

SIKU moja baada ya kuenea taarifa ya kuuawa kwa mfanyabiashara wa madini, Musa Hamis, anayedaiwa kuuawa na askari wa Jeshi la Polisi, Mkoa wa Mtwara, mmoja wa ndugu wa marehemu amedai wakati akifuatilia suala hilo alitakiwa akae kimya au angepewa kesi ya ugaidi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani hapa, mjomba wa marehemu, Salum Ng'ombo, alidai Januari 5, mwaka huu, alimsindikiza mwanawe Kituo cha Polisi Wilaya ya Mtwara baada ya kuelezwa akachukue vifaa vyake.

Hata hivyo, alidai alimtahadharisha wafuatane wasije wakampa fedha bandia na kumfungulia kesi nyingine.

Alidai walipofika kituoni walikutana na askari aliyejitambulisha kwa jina la Grayson, na kumueleza kuwa anamkabidhi mwanawe na kumuomba ahakikishe anarudishiwa vifaa vyake ikiwa ni pamoja na fedha alizokuwa akidai.

"Gryason ninamfahamu alipokuja nikamkabidhi mwanangu akiwa na barua ya mwanasheria baada ya kuona hiyo barua aliwasiliana na mwenziwe na kumwambia kuna barua kutoka kwa mwanasheria wa serikali inataka kijana arudishiwe mali zake," alidai Ng'ombo.

Alisema baada ya muda kijana wake alifikishwa katika chumba cha mahojiano na alikaa kwa zaidi ya saa mbili hali iliyompa wasiwasi na kuamua kwenda kuangalia kinachoendelea. Alisema alipofika kwenye chumba hicho alimkuta mjomba wake akiwa amekalishwa chini hali iliyomfanya ahoji kinachoendelea wakati aliitwa kwa ajili ya kuchukua mali yake.

Vile vile, alidai siku hiyo hiyo saa nane mchana alirudi kituoni na kuomba ampatie chakula ndugu yake, lakini hakufanikiwa na badala yake akaambiwa na mkuu wa upelezi wilaya kuwa aondoke eneo hilo vinginevyo atapewa kesi ya ugaidi.

Ng'ombo alidai siku ya pili alipata taarifa kuwa kuna mtu ameuawa na hakutilia maanani kama ni mjombake, hadi Januari 7, alipoenda kwa Mkuu wa Upelezi mkoa kwa ajili ya kufungua faili la kumtafuta nduguye pamoja na mali zake.

Alisema akiwa kwa RCO, wakati anatoa maelezo na mama wa marehemu, wakaelezwa kuwa suala hilo limehusisha mpaka ofisi ya mwanasheria wa mkoa kwa na kwamba kutakuwa na tatizo na kuombwa wavute subira lifuatiliwe.

### Mama Musa

Mama wa Musa, Hawa Bakari, akizungumza nyumbani kwa ndugu zake, alisema kama sheria ingefuatwa kwa wakati mwanawe asingefia mikononi mwa polisi.

Alisema kwa mara ya kwanza polisi walipofika katika kijiji cha Luponda, Wilaya ya Nachingwea, walitaka waonyeshwe fedha zilipowekwa na kijana wake aliposita kuwaonyesha walimuelekezea bunduki.

Aliomba serikali isaidie haki kutendeka ikiwa ni pamoja na fedha za mtoto wake kurejeshwa.

### IGP Sirro

Juzi Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Mark Njera, akihojiwa na chombo kimoja cha habari aliahidi kulitolea ufafanuzi jana, hata hivyo ha kueleza chochote baada ya kuwa katika vikao na viongozi wa ngazi ya juu wa jeshi hilo wakiongozwa na IGP.

Kwa upande wake IGP Simon Sirro, alipoombwa na waandishi wa habari azungumzie tukio hilo, alieleza kuwa yupo na Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni na kwamba jambo lolote kwa wakati huo atalitolea ufafanuzi waziri huyo.

## Bil.35/- Morocco Square zapatikana

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema kwamba fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi wa Morocco Square, mkoani Dar es Salaam Sh. bilioni 25 zimepatikana.

Kadhalika, imesema inaandaliwa sera ya nyumba ambayo itaondoa mapungufu yaliyoko, ili upangaji wa gharama za pango za nyumba hiyo kuwa shirikishi na halisi ambazo Watanzania wanazimudu.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, aliyasema hayo juzi baada ya kutembelea eneo la mradi huo, akisema matarajio ni kukamilika Juni mwaka huu.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutafanya kuendelea kwa shughuli za maendeleo zilizokwama, ikiwamo kibiashara pamoja na kupendezesha mandhari ya mji.

"Mradi umefikia asilimia 93 ya ujenzi, fedha ilikuwa kikwazo, tutahakikisha mradi unakamilika sasa tunasubiri Wizara ya Fedha na Mipango, kutoa fedha mapema ili ndani ya miezi sita, ukamilike," alisema Ridhiwani.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA: KWA AJILI YA USAMBAZAJI WA VIFAA VYA KAMBI YA MUDA KATIKA MRADI WA EACOP KUMBUKUMBU NA. 0010007422**

Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Total Energies East Africa Midstream B.V. ya nchini Tanzania, inakaribisha mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao kuwezesha uanzishwaji na usimamizi wa vifaa vya kambi ya muda katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpakaChongoleani, MkoawaTanga nchini Tanzania. Urefuwa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi wa EACOP unamtafuta Mzabuni mwenye uzoefu wakutosha ili kuanzisha na kusimamia kambi za muda kandokando mwa Ukanda wa Mkuza wa Bomba la mafuta ili kusaidia mchakato wa utwaaji wa ardhi. Uanzishaji na usimamizi wa Kambi za muda zinazohamishika utajumuisha kwa kiwango cha kawaida:

- Upatikanaji wa maeneo yanayofaa na yanayofikika ili kuanzisha kambi za muda.
- Utoaji wa mahema kwa ajili ya mahali pa kuishi kwa watu katiya 30 hadi 50.
- Utoaji wa huduma za usafi wa mazingira (kama vile kusafisha, ufuaji, maji taka, kuoga, vyoo n.k) kwa watu kati ya 30 hadi 50, na kuhakikisha kuna mgawanyo mzuri wa vifaa vya wanaume/wanawake.
- Utoaji wa huduma ya chakula angalau milo mitatu kwa siku, huku milo ya mchana ikitolewa kwa ajili ya kula palepale au kuondoka na chakula. Maandalizi yote ya chakula yatafuata viwango vya juu na kuzingatia mahitaji ya kitamaduni.
- Utoaji wa huduma za afya, usalama na ulinzi ikijumuisha ulinzi wa vitu, kinga na udhibiti na usimamizi wa moto, na vifaa vya matibabu/uimarishaji katika maeneo ya Mradi.
- Mfumo wa usimamizi ili kuruhusu utunzaji/uhifadhi wa malazi katika kambi za muda kwa ajili ya timu za EACOP.
- Usimamizi wa aina zote za taka zinazozalishwa kupitia shughuli za kambi za muda.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni yanayoonyesha nia yanakaribishwa kuandika maombi yao kwa kuambatanisha:

- Uthibitisho wa Usajili pamoja na Leseni ya Biashara ya sasa.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Cheti cha mlipa kodi ya mapato (TRA) cha mwaka wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini – OSHA
- Wakati wa kuwasilisha majibu kuonesha nia inasisitizwa sana kuambatisha maombi ya kujisajili kwenye kazidata ya EWURA (LSSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa uzoefu katika uanzishaji na usimamizi wa kambi za muda kwa ajili ya shughuli za viwanda nchini Tanzania.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tarehe **09 Februari 2022** saa **11 jioni** saa za Afrika Mashariki (EAT), Baruapepe inapaswa kuwa **0010007422.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuoesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

166680

HABARI MICHEZO

# MOALLIN SASA KOCHA MKUU KAMILI AZAM

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Mkurugenzi wa Ufundi na Maendelea ya Soka la Vijana wa Klabu ya Azam FC, Abdi Ahamid Moallin, ametangazwa kuwa kocha mkuu wa timu hiyo.

Klabu hiyo imemtambulisha rasmi kocha huyo kwenye mtandao wake wa kijamii wa instagram jana mchana kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Mzambia George Lwandamina aliyeamua kubwaga manyanga na kuvunja mkataba kwa makubaliano ya pande zote mbili baada ya timu hiyo kuwa na matokeo mabaya.

"Tuna furaha kumtangaza Ahamid Moallin kuwa kocha mkuu wa timu yetu kwa miaka mitatu ijayo."

Ilisomeka taarifa iliyotolewa na klabu hiyo kwenye mtandao wake wa kijamii.

**Klabu hiyo pia iliweka picha ya kocha huyo akiwa ameshika jezi, pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Adulkarim Amin 'Popat'.**

Ilionekana ni suala la muda tu kwa Moallim, raia wa Marekani mwenye asili ya Somalia kuwa kocha mkuu, kwani tangu atwae jukumu la kuifundisha timu hiyo baada ya Lwandamina kuondoka Desemba 13, mwaka jana, timu hiyo imekuwa ikifanya vema kwenye michuano mbalimbali, lakini ikibadilika hata kiuchezaji.

Tangu alipoitwa timu hiyo akiwa Kaimu Kocha Mkuu, Moallin ameiongoza kwenye mechi tano za Ligi Kuu, akishinda mitatu na sare moja na kupoteza mmoja.

Ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mbeya City, ikaichapa Ruvu Shooting 4-1, kabla ya kufungwa 2-1 dhidi ya Simba, ikaitwanga Mbeya Kwanza bao 1-0, na Jumamosi iliyopita ikaisasambua Tanzania Prisons mabao 4-0.

Pia aliiwezesha timu hiyo kufika fainali ya Kombe la Mapinduzi, Zanzibar kabla ya kufungwa bao 1-0 dhidi ya Simba kwenye mchezo wa fainali.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Azam, Adulkarim Amin 'Popat' (kushoto), akimkabidhi jezi, aliyekuwa Mkurugenzi wa Ufundi na Maendelea ya Soka la Vijana wa klabu hiyo, Abdi Ahamid Moallin, jana wakati akimtambulisha rasmi kuwa kocha mkuu wa timu hiyo. **PICHA: AZAM FC**

## Taifa Jang'ombe yapania taji la FA

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

TIMU ya Taifa Jang'ome imetamba kuibuka na ushindi katika mechi ya mzunguko wa pili ya michuano ya Kombe la FA ikiwa ili kutimiza lengo lao la kuelekea kunyakua taji hilo linalotoa tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Taifa Jang'ombe itashuka dimbani leo Jumatano kupepetana na timu ya Raskazone ya Ligi Daraja la Pili Mkoa wa Mjini Magharibi.

Akizungumza na gazeti hili juzi, kocha wa timu hiyo, Omar Khamis "Matu", alisema lengo lake kubwa ni kuunyakua ubingwa wa michuano hiyo ambayo unafukuziwa kwa kasi na klabu zote za Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema katika kipindi hiki cha mapumziko timu hiyo iliendelea na mazoezi ya kujiandaa na Ligi Kuu mzunguko wa pili pamoja na michuano ya FA.

"Mapumziko yetu baada ya kumaliza mapinduzi Cup tuliendelea na mazoezi ya kuelekea michuano ya Ligi Kuu pamoja na Kombe la FA, hivyo tumejipanga kupata alama tatu na kusonga mbele katika michuano hii," alisema.

Aidha, alisema katika mchezo huo wa leo, anatarajia kuwatumia wachezaji wake wapya aliowasajili katika kipindi hiki cha dirisha dogo ili kuongeza nguvu.

Hata hivyo, aliwataka mashabiki wa timu ya Taifa ya Jang'ombe kujitokeza uwanjani kwa wingi ili kuipa hamasa timu yao.

# Ndumbaro mgeni rasmi Waitara Trophy

**Na Saada Akida**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika shindano la mchezo wa gofu (Waitara Trophy) la kutambua mchango mkubwa wa Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali George Waitara, katika Klabu ya Gofu ya Lugalo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Klabu ya Jeshi ya Lugalo Gofu, Meja Selemani Semunyu, alisema lengo la shindano hilo maarufu kama Waitara Trophy, ni kutambua juhudi za muasisi wa Klabu ya Lugalo Gofu, mstaafu Jenerali Waitara.

Alisema shindano hilo litafanyika Jumamosi wiki hii katika viwanja vya Lugalo Dar es Salaam na kwamba tayari idadi kubwa ya wachezaji wamejitokeza kushiriki.

"Maandalizi yanaendelea vizuri, hali ya mvua imeendelea kuboresha viwanja kuelekea shindano hilo la kutambua juhudi za muasisi wa Klabu ya Lugalo Gofu,"alisema Semunyu.

Alisema zaidi ya wachezaji 100 watakaoshiriki shindano hilo wanaendelea kujiimarisha, hivyo wanatarajia kuwapo kwa ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja anahitaji kupeleka ushindi katika klabu yake.

"Hili shindano litakuwa na ushindani kutokana na klabu shiriki na mchezaji mmoja mmoja kujiandaa vizuri," alisema Semunyu.

Alisema washiriki wasiwe na hofu kutokana na wingi wa waliojitokeza, kwa sababu ndani ya klabu hiyo kuna viwanja vingi vitakavyomudu wachezaji wote kucheza.

Semunyu alitaja klabu zitakazoshiriki shindano hilo la "Jonnier Walker Waitara Golf Trophy" kuwa ni Dar es Salaam Gymkhana, Arusha Gymkhana, Morogoro Gymkhana, Moshi Tpc, Mufindi na Seacleaf kutoka Visiwani Zanzibar.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GERRARD AMUWANIA GOMEZ
KOCHA wa Aston Villa na nahodha wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard anavutiwa na mlinzi, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 24. (**Football Insider**)

### UNITED YASAKA KOCHA
MANCHESTER United imeongeza kasi ya kutafuta kocha mpya, huku Kocha Mkuu wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, Erik ten Hag wa Ajax, Luis Enrique wa Hispania na Julen Lopetegui wa Sevilla wakitajwa. (**Athletic**)

### AUBAMEYANG AGOMBEWA
KLABU sita za Ulaya zina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 32, ambaye bado yuko nje ya mipango ya kikosi cha kwanza cha Mikel Arteta. (**Mirror**)

### TRAORE UHAKIKA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur ina uhakika wa kukamilisha usajili wa pauni milioni 20 kwa winga wa Wolves kutoka Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 25. Hata hivyo, Wolves wanataka pauni milioni 25 kwa ajili ya mchezaji huyo ambaye mkataba wake unamalizika msimu wa majira ya joto 2023. (**Sky Sports**)

### DIAZ AWINDWA UNITED
KLABU ya Manchester United walikuwa miongoni mwa zilizomchunguza winga wa Colombia, Luis Diaz akiichezea Porto mwishoni mwa juma. Atletico Madrid na Borussia Dortmund pia wanamfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye amefunga mabao 14 katika mechi 18 za Ligi Kuu msimu huu. (**O Jogo**)

### WEST HAM, NICE VITANI
TIMU ya Nice pia inashawishika kutaka kumnunua Jesse Lingard, ambaye anahusishwa na West Ham. (**Foot Mercato**)

### ARTETA AMTAKA LEWIN
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ni shabiki mkubwa wa Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 24, lakini jaribio lolote la kumsajili halitafanyika hadi msimu wa majira ya joto. (**Star**)

### CITY, LIVERPOOL KWA GAKPO
MANCHESTER City na Liverpool wamefanya mazungumzo kuhusu kumsajili winga wa Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 22 kutoka PSV Eindhoven. (**Voetbal**)

### VLAHOVIC AITAKA JUVE
MSHAMBULIAJI wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, ameiambia Fiorentina kuwa anataka kujiunga na wapinzani katika ligi ya Serie A, Juventus. (**90 Min**)

### ARSENAL YASAKA NYOTA
ARSENAL inawafikiria washambuliaji wa Real Sociedad na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22, Lille Jonathan David, 22, na mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin mwenye miaka 24, kama matumaini yao ya kumpata Vlahovic yakifiifia.(**London Evening Standard**)

### NEWCASTLE WAKOMAA NA LINGARD
KLABU ya Newcastle inavutiwa na mshambuliaji wa Manchester United, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29 na kiungo wa kati wa Brighton raia wa Mali, Yves Bissouma, 25. (**Mirror**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA AMTETEA MESSI KUSHINDWA KUNG'ARA PSG

### Anayemkosoa ni mtu ambaye haelewi chochote kuhusu soka kwa kweli...

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Karim Benzema, amesema ni suala la muda tu Lionel Messi kuanza kung'ara katika klabu ya Paris Saint-Germain.

Tangu atue PSG, Messi amekuwa akikabiliwa na majeraha na amefanikiwa kufumania nyavu mara sita pekee katika mechi 16 alizocheza.

Wakati wa mapumziko ya Krismasi, Messi pia alipimwa na kukutwa na COVID-19 nchini Argentina na alizuiliwa kufanya mazoezi binafsi ya kupona kwa zaidi ya mwezi mmoja.

"Huwezi kumkosoa mchezaji kama Lionel Messi, anayemkosoa ni mtu ambaye haelewi chochote kuhusu soka kwa kweli," alisema Benzema katika mahojiano na kituo cha Ufaransa cha Telefoot.

Messi amekosa mechi tatu katika kipindi chake cha mwezi mmoja akiwa hayupo, wakati huo PSG wameendeleza uongozi wao kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Messi akitokea benchi dakika ya 63, akichukua nafasi ya Angel Di Maria alihusika katika ushindi wa mabao 4-0 wa PSG dhidi ya Reims Jumapili akitoa pasi ya goli la tatu lililofungwa na Marco Verratti.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 878

MECHI KALI
KAGERA SUGAR
VERSUS
SIMBA
1 | 5.60
X | 3.09
2 | 1.67

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BALOTELLI AREJESHWA TIMU YA TAIFA ITALIA



**ROME,** Italia

MARIO Balotelli ameitwa kwenye kikosi cha Italia kwa ajili ya kambi ya mazoezi ya siku tatu pamoja na Joao Pedro ambao ni sura mpya ndani ya kikosi hicho cha kocha, Roberto Mancini.

Balotelli hajaichezea timu hiyo ya taifa kwa miaka mitatu, lakini kurudi kwenye kiwango chake kumemfanya aitwe katika kikosi cha wachezaji 35 kinachoanza kambi leo Jumatano hadi Ijumaa pale Coverciano.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amefunga mabao tisa kwa kikosi chake cha Adana Demirspor tangu alipojiunga na miamba hao wa Ligi Kuu ya Uturuki Julai mwaka jana, yakiwamo matatu kwenye mechi nne zilizopita.

Wazaliwa wa Brazil, Joao Pedro na Luiz Felipe ni miongoni mwa wachezaji saba walioitwa ambao hawajawahi kuichezea timu hiyo wameitwa na Mancini ikiwa ni miezi miwili kabla ya kuikabili Macedonia Kaskazini kwenye mchezo wa kapu la kufuzu Kombe la Dunia.

Marco Carnesecchi, Giorgio Scalvini, Nicolo Fagioli, Davide Frattesi na Samuele Ricci pia wameitwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi hicho.

# Mashabiki wafariki uwanjani Afcon

**YAOUNDE,** Cameroon

WATU sita wameripotiwa kufariki na wengine kadhaa kujeruhiwa katika msongamano uliotokea nje ya uwanja kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika nchini Cameroon.

Picha za video zimeonyesha mashabiki waking'ang'ana kuingia kwa nguvu katika uwanja wa Paul Biya uliopo katika mji mkuu Yaounde.

Naseri Paul Biya, Gavana wa Jimbo la Kati la Cameroon amesema kuwa huenda kukawa na idadi zaidi ya waathirika, kwa mujibu wa Shirika la Habari la AP.

Ripoti nyingine imeeleza kuwa watoto kadhaa walikuwa wamepoteza fahamu.

Uwanja huo una uwezo wa kuchukua mashabiki 60,000, lakini kwa sababu ya masharti ya kuzuia maambukizi ya corona, ulipaswa kupokea asilimia 80 tu.

Maafisa wa mechi waliripotiwa wakieleza kwamba watu wapatao 50,000 walikuwa wakijaribu kuingia ndani ya uwanja huo.

Msongamano katika lango la uwanja ulisababisha "vifo vya watu sita na wengine kadhaa wamejeruhiwa," aliripoti mtangazaji wa Kituo cha Televisheni cha Taifa, CRTV.

Nick Cavell, mzalishaji wa vipindi wa BBC Afrika, alikuwa katika mechi na amesema kwamba ilionekana taarifa ya mkanyagano haikuwafikia umati wa watu hadi taarifa iliporipotiwa kwenye mitandao ya kijamii.

Muuguzi Olinga Prudence aliliambia Shirika la Habari la AP kwamba baadhi ya majeruhi walikuwa katika "hali mbaya".

Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limesema katika taarifa yake kwamba kwa sasa "linachunguza hali na kujaribu kupata taarifa zaidi za kile kilichotokea".

Mechi ya mwisho ya 16 baina ya Cameroon na Comoro, ilichezwa licha ya tukio hilo na ilimalizika kwa ushindi wa wenyeji 2-1.

,152,880 JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/01/22 | 18:00 | Amorebieta vs Girona | 2.80 | 3.09 | 2.50 |
| 02. 29/01/22 | 18:00 | Tranmere vs Forest Green | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 03. 29/01/22 | 18:00 | Oldham vs Rochdale | 2.80 | 3.25 | 2.41 |
| 04. 29/01/22 | 18:15 | Nancy vs Amiens | 2.52 | 3.16 | 2.77 |
| 05. 29/01/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Almeria | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 06. 29/01/22 | 23:00 | SBV Excelsior vs Emmen | 2.56 | 3.49 | 2.46 |
| 07. 30/01/22 | 16:30 | Vicenza vs Alessandria | 2.66 | 3.05 | 2.66 |
| 08. 30/01/22 | 18:30 | FC Sion vs Grasshoppers | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 09. 30/01/22 | 18:30 | FC Vizela vs Vitoria Guimaraes | 2.90 | 3.20 | 2.47 |
| 10. 30/01/22 | 19:00 | Cardiff vs Nottingham | 2.55 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 30/01/22 | 20:30 | PAOK vs Olympiakos | 2.61 | 3.10 | 2.71 |
| 12. 30/01/22 | 23:00 | Lens vs Monaco | 2.77 | 3.26 | 2.46 |
| 13. 30/01/22 | 23:00 | Ponferradina vs Tenerife | 2.42 | 3.11 | 2.91 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 26/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2581 | Ratchaburi vs Muang Thong Utd | 2.18 | 3.47 | 2.84 |
| 14:00 | 3202 | Nakhon Ratchasima vs Chiangrai Utd | 2.40 | 3.13 | 2.75 |
| 15:30 | 2813 | Asil Lysis vs EN Paralimni | 9.43 | 4.71 | 1.28 |
| 15:30 | 3449 | Omonia Aradippou vs Karmiotissa | 7.31 | 4.23 | 1.38 |
| 15:30 | 3669 | Als Omonia vs Ermis Aradippou | 7.13 | 3.95 | 1.42 |
| 15:30 | 4594 | Alshoulla vs AL Ain | 2.01 | 3.13 | 3.52 |
| 16:00 | 1425 | Rhodos FC vs Kallithea FC | 3.43 | 2.70 | 2.28 |
| 16:00 | 2014 | Kagera Sugar vs Simba | 5.60 | 3.09 | 1.67 |
| 16:00 | 3042 | Kifisias vs Irodotos | 1.25 | 4.82 | 10.60 |
| 16:00 | 3342 | SKODA Xanthi vs Apollon Larisas | 1.20 | 5.37 | 12.47 |
| 16:00 | 3718 | Zanaco vs Green Eagles | 2.33 | 2.74 | 3.27 |
| 16:00 | 3766 | Ergotelis vs Kissamikos | 2.08 | 2.99 | 3.52 |
| 16:30 | 5531 | Persita Tangerang vs Persija Jakarta | 5.39 | 3.61 | 1.57 |
| 17:00 | 2342 | Bengaluru FC vs Chennaiyin FC | 1.47 | 4.24 | 5.39 |
| 17:00 | 5111 | Ethnikos Achnas vs Doxa Katokopia | 2.09 | 3.13 | 3.32 |
| 18:00 | 1330 | Shooting Stars vs Kwara United | 1.74 | 3.08 | 5.01 |
| 18:00 | 1955 | Hajer Club vs Ohud Medina | 2.65 | 3.03 | 2.55 |
| 18:00 | 2799 | Sudtirol vs Triestina | 1.67 | 3.51 | 5.34 |
| 19:00 | 4041 | Ivory Coast vs Egypt | 2.25 | 2.97 | 3.47 |
| 19:30 | 2757 | Olympiakos vs Panetolikos | 1.21 | 5.57 | 10.57 |
| 20:45 | 4117 | Zulte Waregem vs OH Leuven | 2.66 | 3.55 | 2.40 |
| 20:45 | 5195 | Eupen vs Standard Liege | 2.96 | 3.40 | 2.26 |
| 21:00 | 1157 | Saarbrucken vs Borussia Dortmund II | 2.17 | 3.39 | 3.09 |
| 21:00 | 2171 | Sliema Wand vs Balzan Youths | 5.61 | 3.87 | 1.51 |
| 21:00 | 2592 | Lamia vs Aris Salonica | 3.23 | 3.09 | 2.14 |
| 21:00 | 2981 | Verl vs Meppen | 2.37 | 3.39 | 2.75 |
| 21:00 | 3188 | US Quevilly Rouen vs Amiens | 2.81 | 3.15 | 2.46 |
| 21:00 | 3204 | Hamrun Spartans vs Birkirkara | 1.99 | 3.47 | 3.23 |
| 21:00 | 3290 | Angers vs St Etienne | 2.19 | 3.24 | 3.34 |
| 21:00 | 4399 | Duisburg vs Magdeburg | 3.82 | 3.48 | 1.88 |
| 21:00 | 5020 | Ucam Murcia vs Linense | 2.13 | 3.13 | 3.22 |
| 21:00 | 5107 | TSV Havelse vs Wehen | 3.94 | 3.64 | 1.81 |
| 21:00 | 5250 | Zwickau vs Eintracht Braunschweig | 3.23 | 3.28 | 2.15 |
| 21:30 | 2558 | UD Tomares vs Cabecense | 1.91 | 3.38 | 3.57 |
| 21:30 | 4141 | Audax Rio EC RJ vs Nova Iguacu RJ | 3.32 | 3.13 | 2.09 |
| 22:00 | 1117 | Juventude RS vs Internacional | 3.85 | 3.08 | 1.94 |
| 22:00 | 1536 | Mali vs Equatorial Guinea | 1.64 | 3.41 | 5.94 |
| 22:00 | 2475 | La Equidad vs Once Caldas | 2.07 | 3.09 | 3.43 |
| 22:00 | 2688 | Lecce vs Vicenza | 1.36 | 4.72 | 7.66 |
| 22:30 | 1319 | Motril vs Jaen | 1.81 | 3.48 | 3.86 |
| 22:45 | 2638 | Rangers vs Livingston | 1.16 | 6.73 | 15.84 |
| 22:45 | 2647 | Motherwell vs Hibernian | 3.15 | 3.15 | 2.27 |
| 22:45 | 3111 | Hearts vs Celtic | 4.53 | 3.69 | 1.71 |
| 22:45 | 4221 | St Johnstone vs Dundee FC | 2.34 | 3.01 | 3.16 |
| 22:45 | 4223 | Dundee Utd vs Ross County | 2.35 | 3.21 | 2.96 |
| 22:45 | 4511 | Sporting Lisbon vs Santa Clara | 1.38 | 4.34 | 6.94 |
| 23:00 | 1599 | West Bromwich vs Preston | 1.60 | 3.74 | 5.31 |
| 23:00 | 4225 | Racing Santander vs Racing Ferrol | 2.01 | 3.18 | 3.47 |
| 23:00 | 4230 | RFC Seraing vs Kfco Wilrijk | 1.98 | 3.59 | 3.44 |
| 23:00 | 5800 | Anderlecht vs Cercle Brugge | 1.61 | 4.03 | 4.82 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MAYELE AFUNGUKA UBORA MAKAMBO, USHINDI YANGA



**Na Mwandishi Wetu**

KINARA wa mabao wa Yanga, Fiston Mayele, amesifu uwezo wa straika mwenzake, Heritier Makambo, akieleza ni mshambuliaji mzuri na anajua kufunga, lakini tatizo ni nafasi tu ndani ya klabu hiyo, huku akiwataka Wanayanga kutarajia makubwa pia kutoka kwa Chiko Ushindi.

Makambo amekuwa akianzia benchi dhidi ya Mayele ambaye ameonekana kuwa chaguo la kwanza kwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mtunisia Nasreddine Nabi. Lakini Mayele ambaye hadi sasa ana mabao sita, moja nyuma ya kinara wa mabao wa Ligi Kuu Bara kwa sasa msimu huu, Riliants Lusajo, amemwambia mwandishi wetu kuwa hana hofu kuhusu uwezo wa Makambo kwani anao uwezo mkubwa wa kufunga.

"Makambo ni mchezaji mzuri, mshambuliaji mzuri na anajua kufunga, mlimuona amefunga mabao matatu kwenye Kombe la FA, unajua timu yetu ina wachezaji wazuri, ukipata nafasi lazima uitumie," alisema.

Kuhusu Chiko Ushindi, ambaye amesajiliwa katika usajili wa dirisha dogo Januari hii, huku wiki iliyopita akicheza mechi yake ya kwanza Ligi Kuu Bara akitokea benchi wakati Yanga ikishinda bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Mayele alisema anamjua vema na kwamba ni mchezaji mzuri.



# Hitimana na hesabu za kuing'oa Ruvu FA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amesema ameanza kukiandaa kikosi chake kuhakikisha kinafanya vizuri dhidi ya Ruvu Shooting katika mchezo wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Hitimana alisema mchezo huo ni muhimu ili kuvuka hatua hiyo ya 32 na ni mgumu kwa kuwa michuano hiyo inachezwa kwa mtindo wa mtoano na timu inapofungwa hutoka.

Alisema kazi kubwa anayoifanya ni kuimarisha kikosi chake kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo ili kusonga mbele katika hatua ya 16-bora.

"Tunafanyia kazi mapungufu ya kikosi chetu, kujiimarisha kila idara ikiwamo ushambuliaji na ulinzi ili kuhakikisha wapinzani wetu hawapati nafasi ya kutufunga na tuweze kutumia vizuri nafasi tunazotengeneza kupata tunachokitarajia," alisema Hitimana.

Alisema ana imani na kikosi chake kufanya vizuri kutokana na mabadilko aliyoyaona ndani ya timu hiyo tangu alipoichukua na sasa imekuwa tofauti kwa sababu wameanza kupata matokeo ugenini jambo ambalo hapo awali halikuwapo.

Michezo

Jumatano Januari 26, 2022

Nipashe



Benzema amtetea Messi kutong'ara PSG UKURASA 21

# PABLO ATAJA MBINU ZAIDI KUTAWALA KAGERA LEO

●●● Baraza asema hatosubiri kidonda kikauke, mashabiki Simba wapata ajali...

**Saada Akida na Christina Mwakangale**

WAKATI leo akikiongoza kikosi chake kushuka dimbani dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema utakuwa mchezo utakaotawaliwa na mbinu zaidi hasa kutokana na ubora wa uwanja kuruhusu mpira kuchezwa.

**Aidha, Pablo amesema baada ya mechi hiyo kumalizika leo jioni, kila mtu atakuwa na nafasi ya kuuzungumzia ulivyokuwa na si vingine tofauti na mechi mbili zilizopita.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema Kagera Sugar ina kikosi imara na inacheza soka la moja kwa moja , hivyo mechi hiyo itaamuliwa kwa mbinu zaidi.

"Hii ni mara ya pili tumekuja Kagera, ya kwanza mechi ilishindwa kuchezwa kutokana na matatizo ya kiafya, ila tunaamini kesho (leo), mchezo utafanyika na tupo tayari kupambana.

"Ninahakika mechi itakuwa nzuri hata kwa kuitazama kwa sababu sehemu ya kuchezea ni nzuri, hivyo kila timu itakuwa na uwezo wa kucheza tofauti na michezo miwili iliyopita," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

Awali, kabla ya kuwasili mjini Bukoba, Pablo aliliambia Nipashe kuwa alichokifanya kwa nyota wake ni kuwajengea kujiamini na mbinu zaidi, kuhakikisha leo wanaifunga Kagera Sugar.

Kikosi hicho cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Simba kiliwasili Bukoba jana asubuhi na jioni kufanya mazoezi ya mwisho katika Uwanja wa Kaitaba huku ikielezwa kitaendelea kuwakosa wachezaji wake wawili, Kibu Denis na Jonas Mkude ambao ni majeruhi.

Wakati Pablo akishuka na mistari hiyo, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, yeye amesema walichokifanya Mbeya City na Mtibwa Sugar dhidi ya Simba, hatakubali kusubiri kidondo kikauke na kwamba wanachotaka ni kukitonesha kidonda mapema.

"Tunataka kukata umeme usipelekwe sehemu fulani, sitangoja kidonda kikauke nitajaribu kukitonesha, tunajua tukisubiri kikauke itakuwa balaa, amekuja 'Kiiza kidogo' na amejaribu kuweka vikao na wachezaji wenzake, hivyo nitajaribu kutoka na pointi tatu," alisema Baraza.

Katika michezo miwili ya mwisho iliyopita, Simba ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya kabla ya kulazimisha sara tasa dhidi ya Mtibwa Sugar katika Dimba la Manugu, Turiani nje kidogo ya mji wa Morogoro.

Katika hatua nyingine mashabiki wa Simba kutoka tawi la 'Wekundu wa Chalinze' waliokuwa wakisafiri kuelekea Kagera kwa ajili ya kuisapoti timu yao, wamepata ajali katika Wilaya ya Kahama Kijiji cha Wendele majira ya saa nane mchana jana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari ya Simba jana ilieleza: "Idara ya Habari imezungumza na Mwandishi wa Habari wa JFIVE Online TV, Ernesto Eliud, ambaye alikuwamo kwenye gari hilo, amesema watu sita wamejeruhiwa ambao ni wanaume wanne na wanawake wawili akiwamo shabiki wa Simba aitwaye Big wa Chalinze.

"Kwa sasa majeruhi wote wamepelekwa Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa matibabu zaidi. Klabu ya Simba inatoa pole kwa wote waliopatwa na madhila hayo na tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu wapate nafuu ya haraka."

Hata hivyo, licha ya ajali hiyo kutokea tangu jana saa nane mchana, Nipashe lilipomtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, majira saa 11:09 jioni kutaka kujua undani wa ajali hiyo, alisema: "Nimeisikia hiyo ajali kama mlivyosikia (waandishi), eneo la ajali inasemekana hakuna mawasiliano."

## POLENI...




Basi lililokuwa limebeba mashabiki wa Simba tawi la Wekundu wa Chalinze, baada ya kupata ajali jana majira ya saa nane mchana katika Kijiji cha Wendele wilayani Kahama. **PICHA: MTANDAO**

## Kocha: Yanga wameacha jembe

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa zamani wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema kuondoka kwa kiungo Mukoko Tonombe ndani ya klabu hiyo ni pengo, akiongeza kuwa angekuwa yeye asingeshauri hivyo.

Mwambusi aliyewahi kumfundisha mchezaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambaye taarifa zilitoka juzi kuwa amejiunga na Klabu ya TP Mazembe, amesema wachezaji kama Mukoko ambao ni wapambanaji ni wachache sana na si hapa nchini tu, bali hata Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

"Yanga wameacha jembe, Mukoko ni mchezaji mwenye nidhamu, mshindani, hapendi kushindwa, halafu ana ushawishi kwa wachezaji wenzake, ana uwezo wa kuwahimiza wapambane na wakafanya hivyo kwa ajili yake, basi ni maamuzi ya klabu. Labda kwa sababu anakosa nafasi ya mara kwa mara ya kucheza na mwalimu anaona anao wengine wa kuwatumia ambao wanampa matokeo hakuna jinsi," alisema Mwambusi.

Alisema kila mwalimu ana falsafa zake na mtazamo wake, lakini huenda klabu imeona ina wachezaji wengi kwenye nafasi moja, kitu ambacho ni gharama na kuziba nafasi kwenye namba nyingi, vinginevyo kulikuwa hakuna ulazima wa Mukoko kuondoka.

"Aina ile ya wachezaji wanahitajika sana kwenye timu, kwa sababu kuna wachezaji wengi ni wazuri wakiwa na mpira, lakini wakipoteza hawapambani kuurejesha kwenye himaya yao, hii si aina ya Mukoko, kwangu mimi naona alikuwa mchezaji aliyestahili bado kuichezea Yanga," alisema.

9 770856 541002 >